SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Spika** Ndugai atoa onyo dhidi ya kauli za Jenerali Ulimwengu

UKURASA 4



**Pogba kukosa mechi zilizobakia za 2021**

UKURASA 21


# Nipashe

Ijumaa Novemba 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580762

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# Mafuta yaliyopo yatosha siku 15

• **Serikali** yaja na mkakati kukabiliana na uhaba wa nishati hiyo... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**WAVUTA BANGI WAWA TISHIO KWA WANAFUNZI**

UONGOZI wa Shule ya Msingi Kilima 'B' katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama...

UKURASA WA 5

**ELIMU CHANJO CORONA YAPUNGUZA WAGONJWA**

HOSPITALI ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iliyoko...

UKURASA WA 5

**WAZIRI ATAJA SABABU RIBA BENKI KUTOSHUKA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, amesema moja kati ya sababu...




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, Dk. Othman Abass Ali, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Machinga sasa watolewa hofu jengo jipya la Kariakoo

UKURASA 3



## KESI YA MBOWE

# Korti yakataa kupokea kielelezo cha Jamhuri

UKURASA 2


**MICHEZO** **PABLO KULIAMSHA SIMBA SC** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (katikati), akiwa ndani ya Mahakama Kuu ya Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sinza, mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayomkabili na wenzake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mafuta yaliyopo yatosha siku 15

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeweka bayana kwamba mafuta yaliyopo nchini kwa sasa yanatosha kwa matumizi ya siku 15, yaani wiki mbili pekee.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam, akitafsiri kwamba ni hali inayoiweka nchi katika hali ya hatari endapo hatua zinazokwenda kuchukuliwa hazitafanikiwa.

"Hivi karibuni kumekuwa na upandaji wa bei ya mafuta na hii inatishia usalama wa nchi. Kwa sasa hivi mafuta yaliyopo ndani ya nchi yanatosha kwa siku 15 tu. ikitokea chochote kama meli haitakuja ndani ya wiki mbili, nchi itakuwa haina mafuta. Hii siyo nzuri kwa usalama wa nchi," alisema.

Dk. Mataragio alikuwa anazungumza wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na shirika hilo kwa waandishi wa habari yaliyolenga kuwajengea uelewa kwenye eneo la miradi ya kimkakati ya mafuta na gesi.

Alisema kumekuwa na ongezeko la bei na serikali ikaamua kufanya uchunguzi kujua sababu za bei kupanda, huku akifafanua hatua za dharura za sasa ni kwamba TPDC imeshaagiza mafuta ambayo yanatarajiwa kuingia nchini wakati wowote.

"Kwenye soko la dunia mafuta yanashuka lakini huku kwetu bei inapanda. Hata yakishuka, hatuoni unafuu, mwaka huu mafuta yalishuka sana bei yakaenda mpaka sifuri lakini sisi bado bei ipo juu," alisema.

Dk. Mataragio alisema ushiriki wa TPDC kwa sasa utasaidia bei ya mafuta isipande kwa sababu wao watakuwa wanayanunua moja kwa moja bila kuwa na njia za mkato.

"Tutahakikisha kunakuwa na mafuta ya akiba ya miezi mitatu, pia tunafikiria kwamba Tanzania tuna bandari, nchi nyingi zilizotuzunguka hazina bandari, wanachukua mafuta kutoka hapa, tukawauzia Malawi, Zimbabwe, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) na Zambia," alisema.

Mjiolojia Mwandamizi kutoka Idara ya Mkongo wa Juu TPDC, Gaston Canuty, alisema shirika hilo lipo katika mikakati yake ya kukabiliana na uhaba wa mafuta nchini na limeanzisha mchakato wa kumpata mbia watakayeshirikiana naye kuagiza mafuta.

Mhandisi Aristides Katto kutoka TPDC, akizungumzia usambazaji wa gesi asilia majumbani, viwandani na kwenye vituo vya kuuzia magari, alisema tangu shirika lianzishwe mwaka 2004, takribani asilimia 60 ya umeme katika gridi ya taifa unatokana na gesi.

"Nyumba zaidi ya 600 zimeunganishiwa gesi, magari zaidi ya 600 makubwa na madogo yameunganishiwa gesi na mengi ambayo yameunganishiwa ni zinazofanya biashara ya UBA na BOLT.

"Futi za ujazo bilioni 596 ndizo zilizotumika hadi mwezi Juni mwaka huu. Kati yake, viwandani ni asilimia 19.1303, umeme asilimia 80.8479, taasisi, magari na nyumbani asilimia 0.0218," alibainisha.

Katto alisema tangu shirika hilo lilipoanza hadi kufikia mwezi Juni mwaka huu, nchi imeokoa dola za marekani bilioni 17.07 (sawa na trilioni 39.1) ambazo zingetumika kuagiza mafuta nje ya nchi.

Vilevile, alisema kampuni binafsi 10 zimepewa ruhusa ya kuweka vituo vya kujaza gesi kwenye magari na moja tayari imeshakamilisha kujenga kituo eneo la TAZARA.

Kuhusu kituo cha gesi kwa mabasi ya mwendokasi, alisema wanatarajia kufungua zabuni ya kutangaza hilo leo na mkandarasi atakayepatikana atakijenga.

## KESI YA MBOWE

# Korti yakataa kupokea kielelezo cha Jamhuri

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imekataa kupokea kielelezo cha upande wa Jamhuri kwa sababu shahidi SP Jumanne Malangahe hakueleza mtiririko kimefikaje kwake.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Jaji Joackim Tiganga baada ya kupitia pingamizi la mawakili wa utetezi, waliopinga kitabu cha kuweka kumbukumbu za washtakiwa kuingia na kutoka Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam kupokewa kwa utambuzi kwa sababu kina upungufu.

Mabishano hayo yalitokea katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu wakati mahakama inasikiliza kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi.

Akitoa uamuzi, Jaji Tiganga alisema shahidi ameeleza vizuri katika ushahidi wake kwamba alitumia kitabu hicho kumtoa mshtakiwa Mohammed Ling'wenya kwa ajili ya kwenda kumhoji na kumrudisha mahabusu.

Alisema shahidi ni mtu sahihi kutoa nyaraka hizo, kama kielelezo hicho kikipokelewa kitaisaidia mahakama katika kutoa uamuzi ikiwamo katika pingamizi la mshtakiwa Ling'wenya kwamba hakuwahi kufika Kituo Kikuu cha Kati Dar es Salaam. Jaji Tiganga alisema shahidi alisema anatambua kielelezo hicho na alieleza jinsi alivyoshughulika na kielelezo hicho.

"Shahidi hakueleza tangu alipoachana na kielelezo hicho Agosti 7, mwaka 2020 kilikuwa wapi, ilikuwa lazima kuwapo na mtiririko lakini hayo hayakuzungumzwa.

"Kielelezo kimemfikia shahidi bila maelezo kimemfikia kwa utaratibu upi, kielelezo kipo katika chumba cha mtunza vielelezo, hakuna mahali ilionyeshwa kilitolewa lini kikafika kwa shahidi. "Shahidi kashindwa kueleza mtiririko wa kielelezo hicho kufika kwake, mahakama hii inakataa kupokea kielelezo hicho, mapingamizi ya mawakili wa utetezi yamekubaliwa," alisema Jaji Tiganga.

Miongoni mwa mapingamizi ya mawakili wa utetezi ni kwamba shahidi hakuwa na sifa ya kuwasilisha kielelezo hicho na hakueleza mtiririko tangu aachane na kielelezo Agosti 7, mwaka 2020 wakati amemaliza kumhoji, kilifikaje kwake.

Baada ya kukataliwa kielelezo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, aliendelea kumhoji shahidi ambapo alidai Ling'wenya akiwa katika chumba cha mashtaka Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam, alikuwa mwenye afya njema na hakuwa na tatizo lolote.

"Nilimchukua mshtakiwa kwa ajili ya kumhoji, nilijitambulisha na kumpa haki zake, alikubali kuandika maelezo akiwa peke yake, alieleza kwa kina namna anavyohusika katika tuhuma za kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

"Baada ya kuandika maelezo aliyapitia na kuridhika, alisaini na mimi nikasaini, si kweli kwamba Ling'wenya hajawahi kufika Kituo Kikuu cha Polisi Dar Salaam kama inavyodaiwa, Agosti 7, 2020 mimi nilimkabidhi mahabusu akiwa na hali nzuri, nilienda kumchukua mimi na kwenda kuandika maelezo na kumrejesha.

"Ninathibitisha niliandika maelezo Kituo Kikuu cha Polisi Agosti 7, 2020, yuko askari ambaye alinikabidhi wakati naenda kuchukua maelezo, hata nilipomrejesha askari huyo alimpokea," alidai SP Jumanne.

Shahidi alidai hakuwahi kumtisha Ling'wenya, alikuwa na ushirikiano na hakuwa na sababu ya kumtisha kwani aliandika maelezo kwa hiari na alisaini.

Shahidi aliomba kutoa maelezo ya Ling'wenya baada ya kuyatambua kwa ajili ya utambuzi na upande wa utetezi haukuwa na pingamizi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

## Wavuta bangi wageuka tishio kwa wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UONGOZI wa Shule ya Msingi Kilima 'B' katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, umeomba serikali kuwaondoa vijana wanaovuta bangi kuzunguka shule hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Apolinary Antony, alisema hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari katika eneo la shule hiyo kwamba baadhi ya wanafunzi wanaokota vipande vya bangi na kuvuta wakati wa kipindi cha mapumziko.

Alisema kuna kipindi vijana wanaovuta bangi kuzunguka shule hiyo walikuwa na tabia ya kuwaingilia mbuzi kimaumbile huku wanafunzi wa kiume wakiiga tabia hiyo kwa kuwakamata wanyama hao wanaofungwa pembezoni mwa shule.

"Mimi mwenyewe nimeshuhudia wanafunzi wakiingilia mbuzi na nilipowabana kwa viboko ili waseme wamejifunza wapi tabia hiyo waliweka bayana kwamba waliona vijana wanaovuta bangi nyakati za jioni katika eneo la shule nao wakaamua kuiga," alisema Antony.

Mwalimu wa takwimu wa shule hiyo, Sofia Mselemu alisema, uvutaji wa bangi unaofanywa na watu wanaookaa katika eneo la shule umewafanya wanafunzi kushiriki katika uvutaji huo hali ambayo imechangia hata wengine kukatiza masomo.

Alisema baadhi ya wanafunzi hususani wa kiume wamekosa nidhamu kwa walimu wao ikiwamo kutowapokea mizigo wanayokuja nayo.

Mselemu alisema wapo baadhi ya watu kipindi cha nyuma walikuwa wakifika shuleni hapo na magari na kuuza dawa za kulevya na wanafunzi walikuwa wakitumiwa kuyasambaza kwa wateja wao, lakini walipambana na tatizo hilo mpaka likaisha.

Kwa upande Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliahidi kupambana na vitendo hivyo ambavyo vinaendelea kwa sasa na kwamba atapeleka polisi ili kuangalia usalama wa mali za shule pamoja na kuwaondoa vijana wanaovuta bangi eneo hilo.



Mgombea Ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Ngorongoro, Emmanuel Shangai (kulia), akichukua fomu kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Dk. Juma Mhina jana, kwa ajili ya kuingia katika uchaguzi mdogo wa ubunge jimboni humo, unaotarajia kufanyika Desemba 11, mwaka huu, baada ya mbunge wa jimbo hilo, William Ole Nasha kufariki dunia hivi karibuni. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Machinga watolewa hofu jengo jipya la Kariakoo

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imewaondoa hofu wafanyabiashara waliokuwa katika Soko Kuu la Kariakoo, kwa kuwaeleza kuwa watarejeshwa katika maeneo yao ujenzi wa jengo jipya utakapokamilika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa kauli hiyo jana bungeni baada ya kuulizwa swali na Mbunge wa Viti Maalum, Nusrat Hanje, kuhusu ujenzi wa soko hilo.

Hanje alisema: "Ramani mpya ya ujenzi wa Soko Kuu la Kariakoo inaonyesha kutajengwa majengo mawili, utaratibu wa kujenga unataka ujenzi wa jengo kubwa uende sambamba na ujenzi wa soko dogo."

"Kwa nini serikali isiweke utaratibu wa kujenga masoko haya kwa awamu ili kuondoa vurugu, lianze soko kubwa wakati soko dogo likiwa bado lipo, likimalizika ndipo waanze na ujenzi wa soko dogo?" Alihoji.

Akijibu, Majaliwa alisema Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa sasa ipo katika zabuni ili ujenzi wa soko jipya uanze katika kipindi kifupi, wafanyabiashara warudi katika maeneo yao.

Alisema baada ya kuungua kwa soko hilo serikali ilifanya jitihada kubwa, mojawapo ni kujilidhisha ajali ile ilitokana na nini.

Majaliwa alisema serikali iliunda timu ya uchunguzi ambayo ilifanya kazi vizuri na ikatoa mrejesho wa nini kilisababisha kutokea kwa tukio lile.

"Lakini kamati ile ilituambia madhara yaliyotokea katika tukio lile. Soko la Kariakoo limezungukwa na makazi binafsi ya watu, pia kuna soko dogo ambalo limejengwa sambamba na soko kubwa.

"Usalama wa soko dogo nao haukuwa mkubwa, kati ya mapendekezo yaliyotolewa na kamati ni pamoja na kuliondoa na kulijenga upya ambalo litafanya kazi zake vizuri."

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. bilioni 34 ambazo zitajenga masoko yote mawili.

"Baada ya soko kuungua tuliwapeleka wafanyabiashara katika Soko la Kisutu na Machinga Complex na masoko ya jirani, lakini wote wameorodheshwa na wanafahamika nani alikuwa wapi.

"Malengo ya serikali baada ya kukamilisha ujenzi katika kipindi ambacho linapaswa kukamilika wale wote waliokuwa katika soko dogo na soko kubwa tutawarudisha na kuwaweka katika nafasi zao," alisema. Majaliwa na kuongeza:

"Kwa kuwa soko dogo tumeliboresha tutajenga la ghorofa mbili hadi tatu, hata wale waliokuwa wanazagaa nje na kukosa mahali tutawaweka katika hilo jengo jipya. Kwa hiyo hata wale waliokuwa Kisutu wanauhakika jengo likikamilika watarudi katika maeneo yao, ninaamini wanaamini serikali yao kuwa tutatenda hivyo na kusimamia kazi hiyo kukamilika."

# USAID yaahidi kusaidia sekta ya ardhi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amekutana na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) nchini, Veeraya Kate, huku shirika hilo likiahidi kusaidia sekta ya ardhi.

Waziri alimwelezea hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuimarisha sekta ya ardhi nchini.

Kate alimtembelea Waziri Lukuvi katika Ofisi za Wizara zilizopo eneo la Mji wa Serikali Mtumba mkoani Dodoma jana, kwa lengo la kujitambulisha.

Katika mazungumzo yao, Waziri Lukuvi alimweleza Mkurugenzi huyo wa USAID nchini kuwa, wizara yake iko katika jitihada mbalimbali kuhakikisha ardhi yote ya Tanzania inapangwa na kupimwa.

Kwa mujibu wa Lukuvi, pamoja na juhudi hizo, wizara yake imeanza pia kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa kutumia mfumo wa kidigitali na kuachana na ile mifumo ya zamani iliyokuwa ikitumia karatasi nyingi, huku ikianza kutoa hati za ardhi za kielektroniki yenye kurasa moja.

"Tunataka kwenda mbele zaidi katika teknolojia ya uhifadhi wa kumbukumbu zetu za ardhi na tumeanza kuscan taarifa zetu za ardhi katika teknolojia na tumeanza pia kutoa hati za kielektroniki kwenye mkoa wa Dar es salaam na Dodoma," alisema Lukuvi.

Naye Katibu Mkuu Wizara hiyo, Mary Makondo, alisema, pamoja juhudi za wizara kuhakikisha ardhi inapimwa vipaumbele pia vimeelekezwa kwenye maeneo ya vijijini ikiwamo kutumia njia rahisi ya upimaji na kutoa hati za kimila ili kulinda maeneo pamoja na kuwawezesha wananchi kiuchumi. "Kwa sasa wizara ya ardhi inafanya jitihada kubwa kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa ili kuepuka migogoro ya ardhi na wakati huo kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na kuiwezesha serikali kupata mapato," alisema.

Kwa upande wake Kate aliunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kupitia Wizara ya Ardhi na kusema kuwa shirika hilo liko tayari kushirikiana na Wizara ya Ardhi kusaidia sekta ya ardhi nchini.

"Nimetembelea mkoa wa Iringa kunakofanyika mradi wa upimaji ardhi wa teknolojia rahisi vijijini na kuona jinsi mradi huo ulivyofanikiwa ambapo niliangalia namna bora ya kusaidia miradi kama hiyo na nimeomba kupatiwa proposal kuhusiana na mafanikio ya mradi," alisema Kate.

Serikali ya Marekani USAID imekuwa ikifadhili miradi mbalimbali nchini katika nyanja za nishati, uhifadhi wa mazingira, huduma za afya ya uzazi na afya ya mtoto, huduma za kukabiliana na malaria na msaada kwa wakimbizi.


**NOTICE/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walio orodheshwa kwenye jedwali hapa chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na benki, kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya minada ya hadhara mali zilizowekwa kama dhamana ya mikopo waliyokopa kwa mujibu wa mkataba husika. Minada itafanyika sehemu mali ilipo, siku na tarehe kama itakavyotangazwa kwenye vipeperushi na gari la matangazo.

| TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 03 DEC 2021 | 10;30 ASUBUHI | ISIHAKA ABDUL CHIBWANA | NYUMBA | TUANGOMA- TEMEKE | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 26 NOV 2021 | 10:30 ASUBUHI | LILLIES KUBAGA( LILLIES DAY CARE) | NYUMBA | MBEZI BEACH | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 26 NOV 2021 | 14;30 MCHANA | FATUMA CHIZENGA | NYUMBA | MANZESE UZURI-KINONDONI | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 03 DEC 2021 | 11;30 ASUBUHI | DAWSON RWEGASIRA BUTEMBE | KIWANJA | MBAGALA KWA NYOKA-TEMEKE | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 03 DEC 2021 | 10;00 ASUBUHI | SAIDI JUMA KIBORE | NYUMBA | MBAGALA NZASA-TEMEKE | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 04 DEC 2021 | 11;00 ASUBUHI | MZEE YUSUPH MWINYI | NYUMBA | CHANIKA MBUYUNI PLOT NO.115 & 116 BLOCK Q | MUDU CO.LTD |
| 26 NOV 2021 | 10:30 ASUBUHI | SULEIMAN S SULEIMAN | GARI | MANZESE-GARI NO T655DEK | AJ RECOVERIES LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa malipo ya asilimia 25% ya fedha taslim papo hapo baada ya nyundo ya dalali, na ndani ya siku 14 toka siku mnada mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 75% ya salio.
2. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo na sehemu ilipo.
3. Mnunuzi atakaposhindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
4. Mali / dhamana zitauzwa kama zilivyo.
5. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba zilizohapo juu au nenda tawi lolote la Letshego bank lililo karibu nawe.

**MKURUGENZI AJ RECOVERIES: 0755214123, WHATSAPP NO: 686153126**
**MKURUGENZI Mopeh Co. Ltd: 0785 335544, WHATSAPP NO: 0785 335544**
**MKURUGENZI MUDU Co. Ltd: 0768672367, WHATSAPP NO: 0752111140**

216567302

HABARI KITAIFA

# Ndugai atoa onyo kauli za Ulimwengu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limempa onyo mwanahabari nguli nchini, Jenerali Ulimwengu, likimtaka achunge ulimi wake kuhusu matamshi yake anayoyatoa dhidi ya mhimili huo.

Akizungumza jana bungeni, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema mwanahabari huyo amekuwa akitoa kauli za kukashifu watu, kitendo ambacho hakipendezi.

Spika Ndugai alisema: "Haipendezi kwa umri wake aongee ovyo ovyo, akikashifu watu haipendezi, akiendelea na sisi hatutaacha kukaa kimya, tutaagiza watu washughulike naye ikiwamo Bunge na Mahakama."

Alisema mwanahabari huyo amekuwa akikashifu watu, anaudhi watu kupitia mitandao ya kijamii na mialiko, akisisitiza ifike mahali uvumilivu ufike mwisho, kwamba "wabunge siyo mazuzu".

Hivi karibuni wakati akifungua wiki ya Azaki jijini Dodoma, Spika Ndugai alitoa kauli ya kuwaonya watu wanaowadhalilisha wabunge kwa kuwaita majina yasiyofaa kama vile mazuzu.

Akiwa katika maadhimisho hayo, Spika Ndugai alisema anakerwa na tabia ya baadhi ya watu kuwaita wabunge mazuzu na kuwataka wajenge utamaduni wa kuheshimiana. "Sio unaitwa Azaki basi unawasema wenzako maneno unayotaka ya ovyo. Tumewahi kugombana na baadhi ya wazee, mzee unatuita jina sisi hatulipendi...Hivi tumekosea wapi kama unamwita mtu jina la Juma anasema mimi jina hilo silitaki.

"Tatizo lako nini? Unang'ang'ania kuita hilo jina, wewe ni nani? Haiwezekani kama mwanadamu akikwambia hiki sina raha nacho, kiache na wewe hukiachi. Kama kweli wewe ni muungwana, mtu wa Mungu utakiacha," alisema.

Spika Ndugai alisema Bunge halina muda wa kubishanabishana na watu wa namna hiyo, akitamba kwamba amechaguliwa na watu 400,000 kuwa mbunge kwa miaka 25 katika uchaguzi mbalimbali na mara mbili amepita bila kupingwa.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Almasi Nyangasa (kulia), akifafanua jambo baada ya kupata maelezo juu ya fursa zinazopatikana katika Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, wakati wa uzinduzi rasmi wa wiki ya maonyesho ya huduma za fedha katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Masoko Mwandamizi UTT AMIS, Grace Ngailo na Ofisa Masoko na Uhusiano, Waziri Ramadhani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bunge lataka sheria ndogo zifumuliwe

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeiagiza serikali kuhakikisha inazifanyia marekebisho sheria ndogo ambazo zimekuwa kero na kandamizi kwa wananchi kwa kuwa zinakinzana na Katiba.

Limesema sheria hizo ndogo zisipoangaliwa kwa umakini zinaweza kuwa mazalia ya kero, bughudha na manung'uniko katika jamii, kwamba zikitungwa ovyo zinaathiri maisha ya watu ikiwamo kufungwa jela na kutozwa faini.

Akiwasilisha bungeni taarifa ya Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo pamoja na kanuni za uvuvi za mwaka 2009, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jasson Rweikiza, alisema sheria hizo zinawahusu Watanzania wote na ni sheria kama sheria zingine na zina nguvu kuliko sheria zinginezo.

Rweikiza alisema sheria hizo zina nguvu kwa sababu zinatoa faini na vifungo pamoja na kuweka zuio na mipaka mbalimbali.

Alisema Katiba ya nchi imetoa maelekezo ya namna gani sheria mbalimbali zitungwe, lakini sheria ndogo nyingi zimetungwa katika mazingira ya kukinzana na katiba.

"Kwa mfano katiba inatoa haki ya kufanya kazi kwa mtu yeyote au kampuni au mtu binafsi, lakini sheria ndogo inasema ukitaka kufanya biashara ya samaki lazima uwe kampuni, sasa hii inakiuka katiba na inapaswa kufanyiwa marekebisho," alisema Rweikiza.

Akitoa mfano mwingine, Rweikiza alisema: 'Kuna sheria ndogo inayoeleza mhifadhi wa misitu anaweza kusitisha kibali cha kushughulika na mazao ya misitu na hana kikomo, inaweza kuwa miaka 10 au 20. Sasa hii sawa, inakinzana na masharti ya katiba na sheria zingine zinazohusika." Rweikiza alitaja sheria ndogo nyingine ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambayo inawahusu ombaomba ambayo ni ya kibaguzi.

Rweikiza alisema: "Unambagua mtu kwa ulemavu jambo ambalo siyo zuri, inaagiza mtu huyo (ombaomba) apelekwe kwao, akabidhiwe kwa mkuu wa mkoa wake, sasa huyu RC ampeleke wapi? Na huyo ombaomba kwao ni wapi?"

Alitaja sheria ndogo nyingine ni katazo la kuvua samaki katika kina cha mita 50 cha ziwa, badala yake mvuvi avue kwenye kina cha mita 20, wakati kina za ziwa ni zaidi ya mita 1,000.

"Unaporuhusu uvuvi ufanyike kwenye kina cha maji ya mita 20 hizi zingine avue nani wakati samaki hawana mipaka? Wanaweza kwenda nchi yoyote na watu wa mataifa hayo wakafaidika na sisi huku tukajinyima," alisema Rweikiza.

Kadhalika, alisema kuna baadhi ya sheria ndogo zinatumika kwa wananchi pasipo kuletwa bungeni, akiwa na angalizo kwamba ni jambo la kufikirisha kwa sababu zikitungwa sheria mbovu, anayelaumiwa ni Bunge.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akijibu hoja hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Jenista Mhagama, alisema: "Ni kweli tuna safari ndefu ya kufanya mageuzi ya kutosha katika uandishi na utungaji wa sheria ndogo.

"Niwaombe sana watumishi wa serikali wanapokuwa katika kazi ya kutunga sheria ndogo, wajue kuwa wamekasimiwa jukumu, hivyo umakini katika utungaji unahitajika kwa viwango vya hali ya juu kabisa."

Jenista aliwataka watumishi hao wajitafakari na kufanya marekebisho ya kutosha kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Sheria.

Jenista alisema serikali itaanza kukagua ili kubaini ni sekta zipi zinaongoza kwa kuwa na sheria ndogo mbovu ambazo zinakataliwa kila siku katika Kamati ya Sheria Ndogo. "Ni lazima katika serikali tujue hizo sekta ambazo kila wakati zinarekebishwa lakini hazina umakini, tuzijue ni zipi zinaongoza. Tukijua hivyo tutajua wanafanya makusudi au wataalamu hao wanaotunga uwezo wao ni wa chini," alisema Jenista.

Alisema serikali imeamua kujitafakari vinginevyo itakuwa ni marudio, kwamba lazima utafutwe mwarobaini wa kumaliza tatizo hilo. "Ninawaagiza watendaji wa serikali wote wanaotunga sheria hizo ndogo kuhakikisha sheria zote zilizopitiwa na kamati ndogo ya sheria zikaonekana na dosari na zile zinazokinzana na Katiba wafanye marekebisho haraka na waziwasilishe kwa mawazili ili zirudi katika sheria ndogo zikiwa zimeondoa ukinzani wa sheria ndogo na sheria mama," alisema Jenista na kuongeza:

"Mimi na mawaziri wenzangu tutakwenda kufuatilia kwenye sekta kuhakikisha tatizo hilo linaondoka."

## Wafanyakazi waishtaki RITA wakidai malipo

**Na Kulwa Mzee**

WAFANYAKAZI 46 wa Kampuni ya Jandu Construction and Plumbing Company wamefungua maombi mahakamani wakitaka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) uwalipe mishahara ya miezi 21 wanayodai.

Maombi hayo yamefunguliwa katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke, wakiomba mwongozo RITA ielekezwe kulipa mishahara yao kama Mahakama Kuu ilivyoelekeza wakati wakala unateuliwa kuwa msimamizi wa muda wa kampuni hiyo.

Maombi hayo namba 495 ya mwaka 2019 yaliyofunguliwa na Florensi Kapara na wenzake 45, yanasikilizwa mbele ya Jaji Ndugulile Mwaseba katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke na yatatajwa Novemba 24 mwaka huu.

Kwa mujibu wa hati ya maombi, pamoja na mambo mengine, inadaiwa kuwa RITA aliteuliwa kuwa msimamizi wa kampuni hiyo iliyokuwa ya marehemu Inderjit Singh Jandu.

Inadaiwa waombaji ni wafanyakazi wa kampuni hiyo mpaka sasa, hivyo waliiomba Mahakama Kuu imteuwe msimamizi wa muda wa kuongoza kampuni hiyo na kuwalipa mishahara yao ambao hawajalipwa tangu Februari 2020.

Inadaiwa kuwa RITA tangu iteuliwe, hajawahi kutimiza wajibu wake ikiwamo kuwalipa mishahara wafanyakazi kama ilivyoelekezwa na mahakama.

"Tunaomba mahakama itoe amri ya kuwalipa mishahara na nafuu yoyote itakayoona inafaa," ilisema hati hiyo ya maombi.

Inadaiwa kuwa pamoja na Mahakama Kuu kuiteua RITA kwa muda kusimamia kampuni ya marehemu, kukusanya na kulinda mali zote za marehemu, madeni, kulipa mishahara, kodi na mengine yote, hadi sasa wafanyakazi hao hawajalipwa.

Wakili wa Serikali, Samwel Mutabazi, akizungumza kwa niaba ya RITA, alidai aliwasilisha pingamizi la awali Novemba 8, mwaka huu, akipinga maombi hayo kusikilizwa mahakamani huko kwa sababu shauri hilo ni la masuala ya kazi, hivyo lingepelekwa mahakama ya kazi kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kuyasikiliza.

Pia alidai hati ya kiapo cha waombaji ni batili kwa sababu hakuna tarehe wala saini zao na ameshawapa waombaji kiapo kinzani dhidi ya maombi yao na pia aliomba tarehe ya kusikiliza pingamizi.

Jaji alisema maombi hayo yanatokana na kesi ya mirathi inayoendelea Mahakama Kuu, hivyo aliomba apewe muda wa kupata maelekezo kutoka kwa Jaji Mfawidhi endapo maombi hayo yatabaki katika mahakama hiyo au yataenda Mahakama Kuu kwenye kesi ya mirathi namba 70 ya mwaka 2019 mbele ya Jaji Edwin Kakolaki.

Jaji Mwaseba aliporejea, aliamuru kesi itajwe Novemba 24 ambapo itajulikana kama maombi yatabakia hapo ama yatahamishiwa kwenye shauri la mirathi lililopo Mahakama Kuu.

## Mwalimu wa chekechea adaiwa kumbaka mtoto

**Na Maulid Mmbaga**

MWANAFUNZI mwenye umri wa miaka minne anayesoma darasa la awali Pugu Kichangani, jijini Dar es Salaam, anadaiwa kubakwa na mwalimu wake, Sekadi Shaban.

Akizungumza jana na Nipashe, mama mzazi wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa), alidai kugundua mabadiliko ya kiafya ya mwanawe Oktoba 7, mwaka huu, baada ya kulalamika kusikia maumivu na kumwomba mama yake ampake dawa kwa kuwa amepata kipele sehemu za siri.

Mama huyo alisema, alimchunguza mwanawe na kuona hali ya tofauti katika maumbile ya mtoto na alipomuuliza alionyesha hofu huku akisema mwalimu shuleni kamfanyia.

"Wakati nikimchunguza mwanangu nilimkuta na michubuko na alama nyeupe kwenye mapaja yake, nilimuuliza nini kimemkuta aligoma kuniambia nikamuahidi kuwa nitampa zawadi, ndipo akanieleza kuwa mwalimu kamfanyia kitu kibaya," alisema na kuongeza;

"Kutokana na maelezo hayo nilimpeleka Hospitali ya Pugu kwa ajili ya kuangalia afya yake, baada ya kufanyiwa vipimo daktari alithibitisha kuwa kafanyiwa kitendo hicho (kabakwa)."

Alibainisha kuwa wakati mwanawe anasimulia tukio hilo, alidai kuwa wenzake wengine wawili wamefanyiwa kitendo hicho na kwamba walifanyiwa kwenye moja ya ofisi.

Aidha, alidai kupeleka majibu ya daktari katika Kituo cha Polisi cha Stakishari na kupewa RB namba STK/RB19770/21 ambayo iliwezesha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ambaye kwa sasa wanasubiri hatua za kisheria dhidi yake.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kichangani, Wambura Mgita, alithibitisha kufahamu tukio hilo baada ya kusikia kwa wananchi na kuamua kufuatilia na kutoa taarifa polisi ili hatua zichukuliwe.

"Kuna watu walinifuata na kujitambulisha kuwa ni ndugu wa mtuhumiwa wakiniomba niwapatie barua ya dhamana, lakini nilikataa kwa kuwa hawakunipa maelezo yanayojitosheleza na mimi sikujua kinachoendelea, baada ya kuondoka alikuja mtu na kunifahamisha kuhusu suala hilo," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mtuhumiwa ameshakamatwa na wakati wowote atafikishwa mahakamani.

# Elimu ya chanjo Uviko-19 yapunguza wagonjwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

HOSPITALI ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iliyoko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, haina mgonjwa wa Uviko-19.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Leonard Subi, akizungumza na watumishi wa afya wa kada mbalimbali, alisema licha ya hospitali hiyo kupokea wagonjwa kati ya 17 hadi 18 kwa siku na kulazwa, hivi sasa hawana mgonjwa kutokana na elimu ya chanjo inayoendelea kutolewa kwa mafanikio.

"Kipindi hiki ni cha neema, tukachanje haraka sana ili hata kirusi kikiingia hakitatuathiri hata kidogo, kwa sababu Watanzania na wana Kilimanjaro watakuwa wamechanja.

"Niwaombe Watanzania tukachanje, tuache mbwembwe, tuache kusikiliza rumors (tetesi), tuwasikilize wanasayansi, tusikilize wizara yetu ya afya, tuwasikilize wataalamu wetu wa afya wanasema nini, na niwaombe sana wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, tusisubiri kuugua." Kwa mujibu wa Dk. Subi, hospitali hiyo ina wataalamu na wanasayansi wa utafiti wazuri, ambao wameshiriki vizuri kwenye uchunguzi anuai wa virusi vya corona nchini.

"Tunayo mitambo ya uchunguzi wa anuai pamoja na kwamba hospitali hii mnaiona iko hapa Siha, Kilimanjaro. Lakini ina uwezo mkubwa wa uchunguzi wa virusi vya corona katika ngazi ya vinasaba.

"Kwa hiyo hatuna shaka, itakapokamilika hii maabara yetu ya kisasa ya kupima virusi vya corona na magonjwa mengine ya mlipuko,

mtaona mambo mengi ya utafiti, lakini tiba itaboreka sana kwa sababu itatumika katika nyanja zote kama maabara yetu ya magonjwa ya maambukizi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Vilevile, Dk. Subi alisisitiza kwamba atasikitika kuona Watanzania wanasahau mwezi wa sita, saba na wa nane, Kilimanjaro hapakuwa salama.

"Mliona misiba mingi, mliona machozi ya watu, mliona watu wanaugua, watu wanaongezeka hospitalini, watu wanataka oksijeni. Tulivyoanza chanjo tumeona mafanikio makubwa sana.

Chanjo hizi hazikingi asilimia 100, lakini zinakinga na kuzuia maradhi kama zilivyo chanjo nyingine kama ndui na surua. Tuhamasishane tukachanje kwa sababu tusipochanja wengi, bado tutaendelea kuathirika na virusi vya corona."

Katika Afrika, nchi ambazo zimefikia kwenye udhibiti bora wa dawa na vifaa tiba, ambazo zinafikia 'maturity level three' ya udhibiti ni Tanzania na Ghana.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya sekta ya fedha na mipango katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwigulu ataja sababu riba za benki kutoshuka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, amesema moja kati ya sababu zinazofanya riba za mikopo ya benki nyingi nchini kuendelea kuwa juu ni uwapo wa idadi ndogo ya wakopaji.

Mwigulu alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya fedha na mipango katika kipindi cha miaka 60, ya Uhuru wa Tanganyika.

Akijibu swali aliloulizwa kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutaka taasisi za fedha kushusha riba za mikopo hadi asilimia 10, alisema kama idadi ya wakopaji itaongezeka basi riba zinaweza kushuka.

"Watanzania wengi bado ni waoga sana kukopa, hata mtu akikopa yuko tayari kukopa kwenye taasisi zake ambazo siyo rasmi na yuko tayari kukopa Sh. 100,000 na kurejesha mara mbili ndani ya mwezi mmoja,"alisema Mwigulu.

Alisema kama watu wengi watabadili mitizamo yao na kuanza kukopa kwa wingi katika benki basi kiasi cha riba kilichopo hivi sasa kinaweza kushuka na kuwezesha upatikanji wa mitaji katika sekta za uzalishaji.

"Leo hii mtu akionekana kakopa hadi watu wake wa karibu wanamsema kuwa kakopa kila sehemu na kumuona kama alichokifanya kuwa ni kitu cha ajabu sana,"alisisitiza Mwigulu.

Aidha, alisema kikwazo kingine ni elimu ya nidhamu ya fedha kwa wakopaji, kwani wengi wao wamekuwa wakichukua fedha na kwenda kutumia katika mambo ambayo hayana tija.

"Mkopo akikopa mwanamume na mama akajua basi kuna kitu kitafanyika, lakini mama asipojua basi fedha hizo zimepotea. Mnaweza kujikuta pale nyumbani kama ameweka hati ya nyumba basi mnabebewa sturi zenu, lakini akikopa mama mkopo huo utafanya kitu.. akina mama wana nidhamu sana ya fedha za mikopo,"alisema.

Mwenendo ukuaji wa Uchumi

Kuhusu ukuaji wa uchumi, alisema tangu Uhuru Tanzania imepitia katika nyakati mbalimbali za mafanikio ya kiuchumi pamoja na changamoto kadhaa zikiwamo ukame katika miaka ya mwanzoni mwa 1970 na 2012.

Vilevile, mdororo wa uchumi wa mwaka 2008, vita vya Kagera mwaka 1978 pamoja na ugonjwa wa UVIKO mwaka 2020.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia mikakati mbalimbali iliweza kujikwamua kutokana na magumu hayo iliyopitia na hii iliwezesha katika historia ya Tanzania kutokuwa na ukuaji hasi wa uchumi (recession) tangu Uhuru.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru ulikuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali, lakini haujawahi kufikia ukuaji hasi.

Nchemba, alisema mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2019.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusifanyie mzaha maji

**HIVI** karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitoa taarifa ya kuongezeka kwa joto na kuchelewa kwa mvua kutokana na jua la utosi, huku kukiwa na kasi ya mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, TMA ilitaja mikoa ambayo imekithiri kwa joto ni Kilimanjaro yenye nyuzi joto 36.4 ikiwa ni ongezeko la nyuzi joto 4.6, Dar es Salaam nyuzi joto 33.8 ikiwa ni ongezeko la 2.2 na Ruvuma 34.

Siku chache baadaye Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), ilitangaza kuwapo kwa mgawo wa maji, na imeshatoa ratiba ya muda gani maji yatakuwa yanatoka sehemu gani.

Pia Mamkala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Moshi (MUWSA), ilisambaza ujumbe kwa wateja wake ikiwataka kutumia vizuri na kuhifadhi maji kwa kuwa yamepungua kwenye vyanzo vyake kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mgawo wa maji umeshaanza kama sehemu ya hatua za kukabiliana na tishio hilo, huku maeneo mengine yakikaa kwa takribani siku tatu hadi nne bila maji, na sasa biashara ya maji imerejea, ambapo walanguzi wanautumia mwanya huo kujipatia fedha.

Baadhi ya maeneo bei ni kati ya Sh. 200 na 500 kwa dumu, na wanaoumia ni wananchi wa kipato cha chini, ambao hawana vyombo vikubwa vya kuhifadhi maji kwa muda mrefu na sasa wanatakiwa kununua.

Juzi Waziri wa Maji, Juma Aweso, akizungumzia mafanikio ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, alisema moja ya kero zinazoikabili mamlaka za maji ni upotevu wa maji kwa kiasi kikubwa.

Alisema kiasi cha upotevu kinakadiriwa kuwa asilimia 20, na kwamba kiasi kikubwa kinapotea kutokana na wizi kwa kuwa kuna viwanda, nyumba za biashara na binafsi wameunganishiwa maji na hawalipi bili kwa mamlaka.

Licha ya wizara husika kueleza hasara wanayoipata kutokana na upotevu wa maji, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanywa na mamlaka hiyo kwa kuwa maji yanayopotea kwa kumwagika ovyo ni mengi sana.

Mathalani, ni kawaida kuona bomba la maji limepasuka na yanamwagika, mteja au mtu yeyote haruhusiwi kugusa na anapowajulisha wahusika huchukua hata siku mbili au tatu hadi wafike na kuziba.

Maji yanaendelea kumwagika kiwango ambacho kingejaza tangi la lita 2,000 au zaidi na kwa mwenye familia ya wastani angetumia kwa zaidi ya mwezi mmoja.


Ni lazima mamlaka ziwekeze nguvu kudhibiti upotevu wa maji kwa kuvuja, ambayo mengi huishia ardhini na machache kuonekana juu ya ardhi, bila hivyo ni kuendelea kupata hasara ambayo ingeweza kuokolewa kwa kuboresha miundombinu na kuchukua hatua madhubuti.

Hali hii inatufundisha mambo mawili kwamba kama nchi tunatakiwa kuendelea na jitihada za kupanda miti na kutunza vyanzo vya maji.

Ni muhimu kasi ya kuwafundisha wananchi umuhimu wa kuvuna na kutunza maji ya mvua ili yasaidie nyakati za kiangazi kama sasa, ingawa wengi hawafanyi hivyo.


Upo uwezekano wa kutunza maji mengi ya mvua, lakini bado nchi haijaweza kufanikisha hilo na sasa hali hii imekuja ili kukumbusha umuhimu wa kihifadhi maji kwa ajili ya nyakati zijazo.

Wananchi wanaoumia ni wa kipato cha chini kwa kuwa badala ya kutafuta fedha ya chakula, sasa wanatakiwa kununua maji ya kutosheleza mahitaji ya usafi wa mwili na nguo, pamoja na shughuli nyingine za nyumba. Lakini, lazima kuwe na elimu sahihi ya matumizi ya maji ili tuyatunze kwa ajili ya matumizi mengine.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmin Protace

# Serikali ivalie miwani mikopo hii yenye ajenda siri kwenye vikundi

**KATIKA** eneo la fedha hivi sasa kuna huduma kila mahali za mikopo. Kunatajwa idadi ya wakopaji ni wachache, huku wanaokopesha ni wengi.

Ni jana tu nilisikia kauli kutoka mamlaka ya kiserikali ikitolewa kuhusu picha ya mikopo ilivyo nchini. Ni kweli hata tukifuata tathmini ya macho, inshallah! Hali si mbaya sana kama unataka mkopo, upo unaelea sehemu nyingi.

Ukienda hivi na kule, taasisi za kukopesha kibao, Saccos na za aina nyinginezo. Hapo sipendi kuwazungumzia sana wasio rasmi. Kinamama kwetu vicoba ndio kila mtaa na idadi yake kwa kweli si haba, zimesheheni.

Katika maisha, nikiri mkopo sio neno geni hata kidogo. Limekuwa likitajwa sana katika taasisi za fedha au mikopo na kutoka kwa watu wanaokopeshana na wataalamu wanasema, unapotoka kuendelea, jitahidi kukopa, halafu ujibane kulipa.

Shida inaangukia katika 'vigezo na masharti na miba ya riba inayoumiza, hata mamlaka za kiserikali zikipaza sauti kuangalia namna gani inaweza kupungua.

Tunapozungumzia mkopo tunamaanisha mtu anachukua na atatakiwa kuurejesha ukiwa na riba ndani ya muda waliokubaliana. Tunaona katika benki wanatoa mikopo ambayo inawasaidia waliokopa.

Serikali pia imekuwa ikitoa mikopo kwa makundi mbalimbali ikiwa ni sera rasmi, huduma hiyo ikipitishiwa mathalan kwenye halmashauri, lengo ni kuwawezesha walio na kipato kidogo kuinuka kiuchumi.

Katika mikopo ya aina nyingi, hivi sasa tuzungumzie hii ambayo inatolewa na taasisi fulani za kifedha kwa wanawake, mara moja kwa wiki, hapa jijini Dar es Salaam, tuliko.

Ikoje? Kwa kuzoea uzoefu wa mahali hapo, kwa kweli mikopo hiyo haijaweza kuwasaidia wanawake zaidi ya kuwakandamiza. Jinsi ya kuipata kwanza utashiriki darasa, utajadiliwa na wakitaka kukupa wanatembelea kwako waone mali za mkopaji endapo atashinda, vigezo atapigiwa simu kwa ajili ya kupatiwa mkopo.

Sasa kinachowakuta kinamama wengi ni kushindwa kuchukua mikopo hiyo, kutokana na kushindwa kukubaliana na viongozi kama vile mwenyekiti, katibu na mwalimu. Ni aina ya makubaliano ambayo iko nje ya yaliyo rasmi kwa mwenyekiti, katibu na mwalimu wao ndio wanapata mikopo.

Mkazi wa Manzese, Dar es Salaam, ana simulizi yake kwamba mkewe aliomba mkopo kupitia taasisi inayotoa mkopo na akafanya mafunzo ili apatiwe hitaji hilo.

Anasema wanaotoa mikopo walifika hadi nyumbani kwake, wakaangalia mali zilizopo katika nyumba yao na wakasema wameridhishwa, wakimwahidi wangempigia simu, amefanikiwa kupitishwa kupata mkopo wa Sh. 500,000.

Anasema baada ya siku mbili mkewe alipigiwa simu akiambiwa kikundi mkopo upo tayari kinachotakiwa ni kutoa fedha shilingi 30,000 kwa kiongozi, shilingi 15,000 kwa katibu, shilingi 15000 mwalimu shilingi 20,000, halafu Sh. 60,400 inabaki kama akiba.

Hapo ndipo akaja na kiulizo hadi kufikia kutoa pesa hizo zote, haja ya mkopo tena bado ipo? Sasa wakichukua hizo pesa, mkopaji anabaki na nini? Wakafikia makubaliano na mkewe wasichuke fedha hizo maana hata uwezekano wa kulipa unakuwa mdogo.

Anasema kitendo cha kuchukua pesa kinabadilisha hata malengo na mustakabali wake wa wazi. Ninachoelewa, mikopo inatolewa kwa ajili ya kuwasaidia wakopaji na kama ni ya kinamama basi ni kwa wanawake hao wakipaji, wakidhi madhumuni maalum waliolenga. Kinyume na hapo ni kuwarudisha nyuma kinamama hao.

Matatizo hayo yanachangia hata wanaochukua mkopo kushindwa kulipa na wengine kuyakimbia makazi.

Anasema mtu ambaye atakataa kutoa pesa huwa hawampitishi jina lake ili asipate mkopo mwingine. Hebu serikali kupitia mamlaka zinazosimamia, zivalie miwani kutumbua jipu hilo lililoko pabaya.

HABARI KITAIFA

# Taa za barabarani usiku shida Mwanza

**Na Richard Makore,**
MWANZA

JIJI la Mwanza linakabiliwa na giza nyakati za usiku, kutokana na taa nyingi kwenye baadhi ya barabara kutowaka usiku na kusababisha tishio kwa wananchi kuvamia na vibaka.

Baadhi ya barabara za Makongoro, Kiloleri, kuelekea Buzuruga na katikati ya jiji taa zilizopo haziwaki wakati wa usiku.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alikiri kuwapo tatizo hilo na kuahidi kuchukua hatua.

Alisema tatizo hilo analijua, na kwamba ameshatoa maelekezo kwa mamlaka zinazohusika ili kuhakikisha taa zote zinafanyakazi wakati wa usiku.

Aliongeza kwamba ataitisha kikao maalum kwa ajili ya kuzungumzia tatizo hilo kupata ufumbuzi wake wa kudumu.

"Nitakuwa na kikao maalum hivi karibuni ofisini kwangu nitawaita wote ili kujua tatizo liko wapi,'' alisema.

Baadhi ya barabara taa zake haziwaki kwa muda mrefu na hakuna mamlaka yoyote inayochukua hatua kumalizia tatizo hilo kwa haraka.

Kutowaka kwa taa hizo kunahatarisha usalama wa wananchi wanaotumia barabara hizo hususani kwa watembea kwa miguu wakati wa usiku.

Katika ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan mwaka huu jijini Mwanza, ziliwekwa taa za muda husasani katikati ya jiji, ambazo zilikuwa zinawaka usiku, lakini baada ya kuondoka ziliondolewa na kubaki giza.



Msanii wa Filamu maarufu duniani wa Bollywood kutoka nchini India, Sanjay Dutt (wapili kulia), akiwa na viongozi wa Africab Group, ambao ndiyo wadhamini wa safari yake hapa nchini, kabla ya kuzungumza na waigizaji wa filamu Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Ziara ya Sanjay hapa nchini ni katika kuunga mkono programu ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kukuza sekta ya utalii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhaba wa maji waziibua mamlaka

**Na Maulid Mmbaga**

KUTOKANA na athari za mabadiliko ya tabianchi, mamlaka za maji katika mikoa mbalimbali zimetangaza uwapo wa changamoto ya kupungua kwa uzalishaji wa maji katika vyanzo vyake.

Katika kukabiliana na tishio la ukame, mamlaka hizo zimesisitiza matumizi sahihi ya maji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA), ilibainisha kuwapo kwa upungufu wa maji katika vyanzo vyake na kuathiri upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo.

Akizungumza na gazeti hili Mkurugenzi wa MUWSA, Kija Limbe, alishauri wananchi katika eneo husika kujenga tabia ya kuhifadhi maji ya ziada kwa kipindi hiki cha ukame ili kukabiliana na changamoto iliyojitokeza.

Alisema tatizo hilo limesababisha uhitaji wa maji kuongezeka katika baadhi ya maeneo, huku akifafanua kwamba kwa wanaotumia lita 40 sasa zimeongezeka hadi 60, hivyo alisisitiza wananchi kuwa na utaratibu mzuri wa matumizi ya maji.

"Wananchi wa Moshi wamezoea kupata maji saa 24 na hawana utaratibu wa kuhifadhi maji, hivyo kutokana na upungufu wa uzalishaji uliojitokeza tunashauri waweke utaratibu wa kuhifadhi hata ndoo tatu ili ziwasaidie kipindi yakiwa hayatoki," alishauri Limbe.

Aliongeza kuwa changamoto kubwa ya maji ipo katika kata 12 zikiwamo Mweka Kaskazini, Mwika na Old Moshi ambazo kuna utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu, huku akidai kuwa mamlaka inaendelea kutimiza majukumu yake katika kushughulikia changamoto hiyo.

Aidha, maeneo mengine yaliyoripotiwa kukumbwa na uhaba wa maji ni mkoa wa Dar es Salaam, ambapo Mamlaka ya Majisfi na Usafi wa Mzingira (DAWASA) Jumatatu ilitoa ratiba ya mgawo wa maji katika baadhi ya maeneo.

# RC alivyowakingia kifua wavuvi

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MKUU wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, amepiga marufuku kukamatwa kasia za wavuvi ndani ya soko la kimataifa la samaki lililoko Kasenda Muganza wilayani Chato.

Uamuzi huo umeonekana kuwahusu moja kwa moja Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wilayani humo ambao wanadaiwa kutengeneza taharuki kwa wananchi kinyume na maelekezo ya serikali.

Mbali na marufuku hiyo, amewataka kwenda kwenye vyanzo vya uharibifu wa misitu kudhibiti ukataji wa miti kwa ajili ya kupasua mbao, kukata mkaa, kuni na kilimo cha kuhama badala ya kuvizia kasia zinazotumiwa na wavuvi wanaokwenda kuvua samaki Ziwa Victoria.

"Wewe ofisa misitu unakumbuka Rais Samia alisemaje...alipiga marufuku kutengeneza taharuki kwa wananchi...najua mnazo sheria zinazowaongoza kutimiza majukumu yenu, lakini kwenye soko hili la kimataifa hakuna msitu kama wananchi wenyewe wanavyosema... naagiza mwende kudhibiti kwenye vyanzo vya uharibifu," alisema Senyamule.

Kauli hiyo ilitokana na malalamiko mengi ya wananchi wa Kata ya Muganza baada ya kuyaelekeza kwa Ofisa TFS, Jackson Amos, ambaye analalamikiwa kukwa kikwazo kwa ya uvuvi kwenye soko hilo.

Mmmoja wa wafanyabiashara wa eneo hilo, Elias Shija, alimweleza Mkuu wa Mkoa huo kwamba soko hilo lipo hatarini kupoteza hadhi yake kutokana na tatizo la kamatakamata ya wavuvi na zana zao yakiwamo makasia.

Alipotakiwa kujibu tuhuma dhidi yake, ofisa huyo TFS alikana kuvamia eneo hilo na kukamata kasia za wavuvi, badala yake akadai anatimiza wajibu wake wa kudhibiti utoroshwaji wa mazao ya misitu ukiwamo mkaa na mbao.

Ofisa mifugo na uvuvi wa wilaya hiyo, Dk. Elfasi Msenya, alisema mapato ya soko hilo kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, serikali kuu ilikusanya Sh. bilioni 1.7 na kwamba mwaka 2020/2021 yalikuwa Sh. bilioni 2.4 zilizotokana na kodi na tozo mbalimbali ikiwamo ushuru wa kusafirisha samaki nje ya nchi.

Kadhalika kwa kipindi cha 2020/2021 halmashauri hiyo ilikusanya Sh. milioni 183 kutokana na shughuli za kiuchumi zinazoendelea kwenye soko hilo.

Mwenyekiti wa soko hilo, Suleiman Said, aliomba serikali kurejesha asilimia 20 ya mapato yanayotokana na makusanyo ili yasaidie kutatua changamoto mbalimbali kwenye eneo hilo.

Soko hilo linatajwa kuwa la pili kwa ukubwa na ukusanyaji wa fedha nyingi za kigeni likitanguliwa na la Kirumba jijini Mwanza.

# Mwalimu matatani kwa madai kuoa mwanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWALIMU wa Shule ya Msingi Itete Kata ya Kirando wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Clarence Mwanakurya (29), amekamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuoa mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 16.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema mwalimu huyo alikamatwa juzi baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kufanya operesheni maalum ya kusaka wanafunzi walioacha shule kwa kupata mimba inayoendelea wilayani humo.

Alisema mwalimu huyo alikutwa akiishi na mwanafunzi huyo aliyemuoa tangu mwaka jana katika nyumba ya serikali inayomilikiwa na Shule ya Msingi Itete na alipohojiwa na kamati alikiri.

Lijualilali alisema mwalimu huyo alimpa mimba mwanafunzi huyo akiwa darasa la saba na wakati anajiandaa kwenda Sekondari ya Kirando alikokuwa amepangiwa kuanza kidato cha kwanza wazazi pamoja na mwalimu huyo walifanya ujanja kumhamishia Sumbawanga Mjini.

Alisema mwanafunzi huyo alikaa Sumbawanga hadi akajifungua na baada ya kujifungua alirudishwa na kuanza kuishi na mwalimu huyo kama mume na mke kwenye nyumba ya Shule ya Msingi Itete ambako anafundisha mwalimu huyo shule ambayo pia mwanafunzi huyo alikuwa akisoma hapo.

Alisema katika Wilaya ya Nkasi kumekuwa na tatizo la wanafunzi wengi kuacha shule kutokana na tatizo la kupewa mimba ambapo mfano waliotakiwa kufanya mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka jana wanafunzi zaidi ya 300 walishindwa.

Alisema kutokana na tatizo hilo, Kamati ya Ulinzi na Usalana imeanzisha operesheni maalum kuwasaka wanafunzi wote walioshindwa kuendelea na masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kupewa mimba.



Meneja Uhusiano wa Wateja wa Benki ya Afrika, Titus Masele (kushoto), akitoa maelezo kuhusu huduma zitolewazo na benki hiyo, kwa mmoja wa wateja aliyetembelea maonyesho ya Wiki ya Huduma za Kifedha, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Da res Salaam jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Madiwani CCM wapendekeza mrithi umeya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Manispaa ya Shinyanga, wamempendekeza Elias Masumbuko kuwania kiti cha Umeya Manispaa ya Shinyanga, kuziba nafasi ya aliyekuwa Meya wa Manispaa hiyo, David Nkulila ambaye alifariki Agosti mwaka huu kwa matatizo ya moyo.

Masumbuko ni Diwani wa Chamaguha Manispaa ya Shinyanga, ambapo kabla ya kushinda udiwani kwenye uchaguzi Mkuu mwaka jana, alikuwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Sanjo kwenye Kata hiyo zaidi ya miaka 15, akichuana na Gulamhafeez Mukadam kwa nafasi hiyo ya umeya ndani ya miaka 10.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Katibu wa CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Agnes Bashem, alisema uchaguzi huo wa kupitisha jina la Meya wa Manispaa ya Shinyanga, kuziba nafasi ya Marehemu Nkulila ulifanyika katika Ofisi za CCM wilaya.

Alisema wajumbe waliopiga kura ni 24 kati ya 25, ambapo Masumbuko alishinda kwa kura 14, dhidi ya Gulamhafeez Mukadam diwani wa Mjini ambaye alipata kura 10, na alishawahi kushika nafasi hiyo.

"Mara baada ya uchaguzi huu wa kura za maoni kumpata Meya wa Manispaa ya Shinyanga kupitia Chama Cha Mapinduzi, jina la Elias Masumbuko litapelekwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, kisha madiwani watampigia kura za Ndiyo au Hapana," alisema Bashemu.

Uchaguzi wa kura za maoni wa kupitisha jina la Meya Manispaa ya Shinyanga, umefanyika baada ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, iliyokutana katika kikao maalum Novemba mwaka huu Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma, na kuwateua Gulamhafeez Abubakar Mukadam na Elias Ramadhani Masumbuko kugombea kiti cha umeya Manispaa hiyo.

# Serikali kuendelea kuboresha sekta ya umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kununua mitambo mikubwa na ya kisasa ya kuchimba mabwawa itakayopelekwa katika kanda zote nchini ili kuendelea kuboresha sekta ya umwagiliaji na kuongeza tija katika kilimo.

"Serikali itaendelea kusimamia eneo la umwagiliaji katika sekta ya kilimo kwa kuwa inatusaidia sana, tumeshatoa fedha kwa ajili ya kununua mitambo na kuboresha iliyopo, eneo hili linatija hasa katika kipindi hiki ambacho hali ya hewa inabadilika."

Alisema hayo jana wakati akijibu swali la George Mwinyisongole, Mbunge wa Mbozi, aliyetaka kufahamu mkakati wa Serikali katika kuboresha kilimo cha umwagiliaji, katika kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu Bungeni jijini Dodoma.

Majaliwa alisema kuwa Serikali itaendelea kulisimamia eneo la umwagiliaji katika sekta ya kilimo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na kwamba fedha hizo zitatumika katika ununuzi wa mitambo mipya na kukarabati mitambo ya zamani.

Pia, alisema kuwa Serikali inatambua huduma ya usafiri inayotolewa na waendesha pikipiki maarufu bodaboda kwa kuwa zimesaidia kupunguza tatizo la usafiri na itaendelea kuboresha huduma hiyo kwa kutoa elimu kupitia Jeshi la Polisi.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Taufiq aliyetaka kujua Serikali ina mkakati gani wa kutoa mafunzo kwa waendesha bodaboda ili kuepukana na ajali za mara kwa mara zinazopoteza nguvu kazi ya Taifa. Waziri Mkuu aliongeza kuwa katika kuhakikisha waendesha bodaboda wanapata elimu, polisi huwafuata katika maeneo yao na kuwaelimisha mambo muhimu ya kuzingatia wawapo barabarani ili waweze kutoa huduma hiyo vizuri.

Alisema Serikali itaendelea na mkakati wa kuwaelimisha vijana hao, lengo likiwa ni kuwawezesha kujua thamani ya kazi yao pamoja na kuzingatia sheria za usalama barabarani. "Wakizingatia sheria watapunguza ajali."

Wakati huo huo, Majaliwa amewataka Watanzania wajiandae kutumia fursa zitokanazo na mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) utakaojengwa mkoani Lindi. "Mradi huu mkubwa na wa kimkakati unakuja kutengeneza fursa nyingi za kiuchumi kwa Watanzania."

## Simu mpya ya Infinix NOTE 11 yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Huduma za Kidigitali, Tigo Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya Simu ya Infinix Tanzania wamezindua simu mpya ya Infinix NOTE 11 Pro.

Imeelezwa kuwa simu hiyo itapatikana kwenye maduka ya Tigo na Infinix nchini kwa bei ya Sh.600,000 na NOTE 11 kwa bei ya Sh.510,000.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja wa bidhaa za intaneti kutoka Tigo, Mkumbo Myonga, alisema:

"Kama kawaida yetu tunaendelea kuwaunganisha wateja wetu katika huduma za kidigitali na leo (jana) kwa mara nyingine tena kwa kushirikiana na wenzetu wa Infinix kuwaletea Infinix NOTE 11 Series, simu bora kabisa ambayo utarahisisha ukuaji wa huduma za kidigitali na intaneti nchini.

"Tunawashukuru washirika wetu Infinix Tanzania kwa kuendelea kuamini njia zetu za usambazaji kwa kina, mtandao mpana wa 4G na msingi wa wateja wetu ambao unatafsiri mauzo ya kifaa cha hali ya juu kinachozinduliwa leo."

Myonga alisema mkakati wao ni kuhakikisha wanasambaza simu janja kote nchini, huku wakihakikisha wateja wanafurahia matumizi bora ya huduma za kidigitali kupitia mtandao wa kasi zaidi wa 4G+ ambao ni mkubwa zaidi nchini, na kwamba wanatoa GB 96 za intaneti bure kwa mwaka mzima.

Ofisa Mahusiano kutoka Kampuni ya Infinix, Aisha Karupa, aliongezea kuwa mfululizo wa INFINIX NOTE 11 umetengenezwa ili kukidhi mahitaji ya kila mtumiaji ndani ya mazingira yake ya kazi, hivyo Infinix inaleta nguvu ya haraka, nguvu ya ufanisi zaidi na utendaji unaotumia mchanganyiko wa kipekee wa teknolojia ya hali ya juu na kwa bei nafuu.

"Infinix NOTE 10 PRO ni moja kati ya simu janja ya kwanza kabisa nchini kuwa na tekinolojia ya Mediatek's Helio G96 ambayo inarahisisha katika suala zima la kucheza Games, Processor ya 120 Hz 6.95'FHD kamera bora kabisa na betri yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa muda mrefu," alisema Aisha na kuongeza:

"Tunawakaribisha wateja wetu wote katika maduka ya Tigo na Infinix kote nchini waweze kujipatia simu hizi mpya zilizoambatana na ofa kibao.

# Warioba akunwa na mafunzo ajira

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amefurahishwa na mafunzo yanayotolewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Private Agricultural Support Sector (PASS) yanayosaidia vijana na jamii kujiajiri.

Jaji Warioba, ambaye ni Mkuu wa SUA, alitoa pongezi hizo katika ziara yake ya siku mbili chuoni hapo, akiwa ameambatana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande na Makamu Mwenyekiti wake, Dorothy Mwanyika.

"Mafunzo hayo yatawasaidia vijana kuwa walimu kwa jamii inayowazunguka na tayari wanakitu cha kufanya ukweli nimefurahi sana kuona vijana kutoka mikoa mbalimbali kama Tabora, Mwanza, Kigoma, Rukwa wakipata mafunzo haya," alisema.

"Mafunzo haya yatasaidia taifa kwa kiasi kikubwa hususani miaka ijayo katika kukidhi mahitaji ya chakula na kuepukana na balaa la njaa kutokana na ongezeko la watu. Wakati nchi inapata uhuru, tulikuwa Watanzania milioni tisa lakini sasa wamefika milioni 60, hivyo tutarajie ongezeko kubwa la watu na uhitaji mkubwa chakula," aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Warioba aliitaka SUA kuongeza elimu kwa upana ili kuwafikia vijana wengi zaidi kwa kuwa mafunzo hayo tayari yameshaleta mafanikio kwa jamii kupitia vijana waliopita ambao walipata mafunzo hayo.

Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alimshukuru Jaji Waroiba kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka minne na mafanikio yalipopatikana.

Prof. Chibunda alisema kuwa wamefanya maboresho makubwa chuoni hapo kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi hususani mashamba ya kujifunzia kwa vitendo ili kujifunza kwa vitendo.

Alisema hatua hiyo imekwenda sambamba na ujenzi wa maabara na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara pamoja na ujenzi wa madarasa ikiwamo maabara mtambuka ambayo inaweza kuchukua wanafunzi 3,200 kwa wakati mmoja.

Pia alisema chuo kimetenga zaidi ya Sh. milioni 450 kwa ajili ya kujenga vitalu nyumba 100 katika kipindi cha miaka mitatu na kwa mwaka huu, wataanza na vitalu nyumba 30 na tayari wamepeleka maombi mahususi kwa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa lengo la kushirikiana kuendeleza wabunifu kwa kujenga vitalu nyumba vingi zaidi.

Katika ziara hiyo, Jaji Warioba alitembelea ndaki mbalimbali zikiwamo za tiba ya wanyama na sayansi za afya, kilimo kwenye shamba la mafunzo, maabara mtambuka, kituo atamizi cha vijana kilichoko chini ya shule kuu ya uchumi kilimo na taaluma za biashara, kitengo cha mifugo Magadu, kitengo cha samaki Magadu na maabara ya sayansi na teknolojia ya chakula.




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo Tanzania, Mkumbo Myonga, akizungumza katika uzinduzi wa simu mpya ya Infinix NOTE 11 Pro na NOTE 11 kwa kushirikiana na Kampuni ya Infinix Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa Infinix, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Shigela sasa aingilia kati shule kukosa vyoo

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, ameingilia kati ukosefu wa matundu ya vyoo kulikosababisha walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mkuyuni, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kutumia choo kimoja kwa ajili ya kujistiri.

Kutokana na hali hiyo Shigela amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kutenga Sh. milioni 11 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo.

Shigela alitoa agizo hilo kutokana na taarifa ya Kaimu Mkuu wa Shule hiyo, Reward Kihedu, kwamba ni muda mrefu walimu na wanafunzi wanatumia choo kimoja kujisaidia.

Hatua hiyo inatokana na ukosefu wa vyoo vya walimu na upungufu mkubwa kwa matundu ya vyoo vya wanafunzi.

Mkuu wa mkoa alifanya ziara kwenye halmashauri ya wilaya hiyo kwa lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi ili kuzipatia ufumbuzi.

Shigela alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu nchini, hivyo ukosefu wa vyoo katika Shule ya Sekondari Mkuyuni unapaswa utatuliwe haraka ili wanafunzi na walimu wasiendelee kutumia choo kimoja.

Alisema wakati halmashauri tayari imetenga Sh. milioni 30 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike wa shule hiyo, lazima watenge Sh. milioni 11 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya shule hiyo.

"Hili halikubaliki, ninaagiza halmashauri kupitia mkurugenzi kutenga Sh. milioni 11 zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule hii haraka iwezekanavyo," alisema Shigela.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Rehema Bwasi, alimhakikishia mkuu wa mkoa kuwa atahakikisha anatenga fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya vyoo shuleni hapo.

Awali, Kihedu alisema changamoto ya walimu kutumia choo kimoja na wanafunzi, inatokana na ubovu wa miundombinu ya choo cha walimu kutofaa kujistiri au vyoo vya nyumba za makazi ya watu zilizopo karibu na Shule.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Shule, Mkuyuni ina zaidi ya wanafunzi ya 900 na zaidi ya walimu 20.

Mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Ahiraph Ally, aliiomba serikali iwasaidie kutatua changamoto hiyo kwa haraka ili kuepusha magonjwa ya mlipuko yanayoweza kujitokeza kutokana na baadhi ya wanafunzi kukidhi haja zao vichakani.

# Neema biashara madini yanukia kwa North Mara

**Na Mwandishi Wetu**

MGODI wa dhahabu wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya Barrick umetaja kampuni 20 ambazo zitashiriki kwenye programu ya maendeleo ya kibiashara.

Utekelezaji huo utafanywa na kampuni ya Kengo Consulting na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). Kampuni hizo zimeorodheshwa kwa kuwa sehemu ya mnyororo wa thamani wa uchimbaji madini kama vile ujenzi, mazingira na biashara ya kilimo. Lengo la programu hiyo ni kuimarisha uwezo wa biashara za ndani ili ziweze kunufaika na fursa zilizopo kwenye sekta ya madini. Aidha, sekta hii inatabiriwa kuchangia uchumi na kufikia pato la taifa la asimilia 10 kufikia mwaka 2025. Rais na Mkurugenzi Mkuu, Mark Bristow, alisema programu hiyo ni udhihirisho wa jitihada endelevu za Barrick katika kujenga uwezo wa watu wa ndani.

"Tangu mgodi huo uanze kufanya kazi, tumekuwa tukishirikiana na wakazi wa maeneo yanayozunguka mgodi wetu kwa kutengeneza fursa za uchumi endelevu kupitia mkakati wa usambazaji wa bidhaa za ndani kwa ajili ya uchumi wa maeneo hayo na taifa kwa ujumla," alisema.

Alisema lengo mahusisi kwa jamii ni kuwekeza kwenye maendelevu endelevu kiuchumi na programu hii ni itachangia kulitekeleza hilo.

"Programu hiyo ya maendeleo ya biashara za ndani italeta mabadiliko makubwa kwenye mnyororo wa thamani kwenye sekta ya madini na tunategemea uwezo wa kampuni yanayoshiriki kuweza kuimarika na kutumia fursa zilizopo kwenye mnyororo huo wa thamani," alisema.

Serikali ya Tanzania iliunda sera ya ushirikishaji wananchi katika maudhui ya ndani ya mwaka 2015 ikilenga sekta ya madini, mafuta na gesi ili kuhakikisha uchimbaji wa madini na mapato yake yanawanufaisha Watanzania. Sera hiyo na kanuni zake inalenga kupanua uwanda wa kibiashara kwenye uchumi wa Tanzania, kutengeneza nafasi za ajira kwa kuhamasisha maendeleo ya taaluma na uwezo wa watanzania kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi nchini.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akikaguliwa kama sehemu ya uzinduzi wa mwaka wa utamaduni wa usalama wa usafiri wa anga, uliofanyika Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: TCAA**

# TCB yawezesha wanawake 300 uelewa masuala fedha

**Na Christina Mwakangale**

ZAIDI ya wanawake 300 wamenufaika na mafunzo ya programu maalum ya kuwajengea uelewa kuhusu fedha, yanayotolewa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB).

Akizungumza na Nipashe kwenye maonyesho ya Wiki ya Huduma za Fedha, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema wiki hiyo ni muhimu kwa umma hasa katika kufahamu matumizi sahihi ya fedha na uhifadhi.

Alisema takwimu zinaonyesha kwamba elimu kuhusu huduma za kifedha kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwamo Tanzania, ni asilimia 42 pekee, akitaja ni idadi ndogo ikilinganishwa na mataifa yaliyoendelea Ulaya.

Moshingi alisema hatua zinahitajika kuongeza uelewa wa huduma hizo ili Watanzania waliopo kwenye shughuli mbalimbali pamoja na wajasiriamali wanufaike na shughuli zao za uzalishaji za kila siku.

"Tuna kazi kubwa kuongeza uelewa wa elimu kuhusu huduma za kifedha kwenye jamii. Ni imani kwamba wiki hii ya elimu itakuwa jukwaa zuri na kiunganisho kizuri na wadau wa sekta ya fedha," alisema Moshingi.

Aliongeza kwamba, benki hiyo imeandaa programu maalumu kwa wanawake kuhusu elimu hiyo kwa mikoa ya Dodoma na Mbeya, na kuifikia mikoa mingine baadae.

Mkurugenzi huyo alibainisha kwamba matumizi sahihi ya fedha na yaliyo rasmi ni muhimu, kwa sababu humsaidia mtu au vikundi vilivyojiunga kupata mikopo kirahisi, kutoka taasisi za kifedha kuziwezesha biashara na shughuli zao kukua.

"Ni ngumu kuitafuta fedha, lakini ni rahisi kuipoteza. elimu ya fedha bado haijawafikia wananchi wengi, waliyonayo ni chini ya asilimia 50, hii inahatarisha ustawi wa jamii kwa sababu fedha ndio kila kitu katika kufanikisha mipango, mfano akiba za vikoba vikundi vidogo ni muhimu katika kusaidia mzunguko wa fedha," alisema.

Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Dk Charles Mwamwaja, akizungumza katika maonyesho hayo baada ya kutembelea mabanda ya taasisi za kifedha yaliyoshiriki, alisema uelewa mdogo kuhusu masuala ya kifedha, unasababisha watu kutofahamu haki zao kwenye sekta hiyo.

Alibainisha kwamba, ushiriki wa wananchi kushiriki kwenye maonyesho hayo ni fursa yao kufahamu mbinu za uhifadhi, akiba, mafao ya kifedha baada ya kustaafu.

"Ni ngumu kuitafuta fedha, lakini ni rahisi kuipoteza. Elimu ya fedha bado haijawafikia wananchi wengi, waliyonayo ni chini ya asilimia 50, hii inahatarisha ustawi wa jamii kwa sababu fedha ndio kila kitu katika kufanikisha mipango, mfano akiba za vikoba vikundi vidogo ni muhimu katika kusaidia mzunguko wa fedha," alisema Dk. Mwamwaja.

Alisema pia mpango wa serikali ni kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili kuwa na mtaala ambao utakuwa maalumu kuelimisha masuala ya kifedha tangu shuleni, akisema kwamba elimu hiyo itaongeza uelewa wa matumizi sahihi ya kifedha kidigitali.

# 'Ukatili kwa wenye ulemavu umulikwe'

**Na Yasmine Protace**

JAMII imetakiwa inapozungumzia masuala ya ukatili wa kijinsia, iangalie pia ukatili ambao umekuwa ukifanywa kwa makundi ya watu wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, katika Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), ambazo hufanyika kila Jumatano na kusimamiwa na TGNP.

" Ukatili wa kijinsia upo, tunapozungumzia masuala ya ukatili makundi ya walemavu nayo yawe yanaangaliwa," alisema.

Aliongeza kuwa ukatili upo kila mahali, na kwamba ukitokea usemwe ili wahusika wachukuliwe hatua badala ya jamiii kukaa kimya, huku matendo hayo yakiendelea.

Catherine Rajabu, ambaye alikuwa mshiriki wa GDSS, ambaye pia ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere ,kichangia mada mada kuhusu mchango wa harakati za jamii katika kubadili mtazamo hasi na ukatili kwa wanawake na watoto, alisema kuwa vijana wengi wanatumia mitazamo hasi katika jamii iliyowazunguka.

" Nguvu ya pamoja itumike ili kupinga masuala ya ukatili " alisema na kuongeza kuwa njia mbalimbali zitumike kuondoa mitazamo hasi.

Msafiri Mwajuma, alisema matukio ya ukatili yapo na baadhi ya watu wamekuwa wakiyaendeleza. Alisema kuna watu wanafanyiwa ukatili, lakini unapojitolea kumsaidia unashangaa huyo huyo unayetaka kumsaidia mwisho wa siku ana malizana na aliyemfanyia ukatili.

Zahara Omary, alisema ukatili upo na baadhi ya watoto wanafanyiwa na baba zao wa kufikia.

Akizungumzia kisa kilichotokea kwao, alisema binti wa miaka 13 alikuwa akifanyiwa ukatili na baba yake wa kufikia. Alisema pamoja na kufanyiwa alikuwa hamwambii mama yake na mwisho wa siku alipata ujauzito na akajifungua mtoto.

" Huyo mtoto alipojifungua vipimo vya DNA (vinasaba) vilifanyika na ikaonekana mtoto ni wa baba yake wa kufikia ," alisema na kwamba wanamsaidia huyo mtoto ili sheria ichumukue mkono wake.

**Aliongeza kuwa ukatili upo kila mahali, na kwamba ukitokea usemwe ili wahusika wachukuliwe hatua badala ya jamiii kukaa kimya, huku matendo hayo yakiendelea.**



Ukurasa 12

TARI Ukiliguru katika 'amshaamsha' kuirejesha zao kimkakati pamba katika enzi zake kutamba



Ukurasa 13

Nendeni kwa usalama barabarani


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 12, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

BAADA KUWEZESHWA NA CHAVITA...

## Kijana athibitisha anaweza; ni seremala kamili, ana familia, nyumba na wapangaji

# JKT yamuitikia Majaliwa; mkonge rasmi kambini Mgambo & Maramba

**Na Renatha Msungu, TANGA**

TANGU serikali ilipoagiza taasisi za umma zikiwamo za jeshi kuchangia uendelezaji kilimo cha kujitosheleza kwa mazao ya chakula na biashara, ili kujiinua kiuchumi.

Hapo ndipo kunakopatikana nafasi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), makambi ya Mgambo na Maramba mkoani Tanga wakijitosa katika zao la mkonge ambalo kitaifa limo katika orodha ya mazao ya kimkakati, kukiwapo zaidi ya ekari 200 kwa ajili ya mazao na mbegu zitakazowatosheleza wao na wananchi jirani.

Kimsingi, mkonge huanza kuvunwa baada ya miaka mitatu tangu ilipopandwa na walinzi hao wa nchi itakuwa zao la biashara kwao, kusaidia kuongeza kipato jeshini.



Katibu wa Kamati ya Kilimo Mkakati, Mifugo na Uvuvi wa JKT, Kanali Peter Lushika, akiwa katika mandhari ya shamba la mkonge la Mgambo JKT. **PICHA: MTANDAO**

### KANALI LUSHIKA

Katibu wa Kamati ya Kilimo Mkakati, Mifugo na Uvuvi wa JKT, Kanali Peter Lushika, anasema katika ekari hizo, saba ni mahsusi wa mbegu.

Anasema hadi sasa mkonge umestawi sana kutokana na uangalizi uliopo kutoka kwa askari vijana wa jeshi hilo na wataalamu wake wa kilimo wanaosimamia kitaalamu.

Kanali Lushika anaiambia Nipashe kuwa kikosi cha JKT Mgambo 835 KJ, kwa sasa wanatekeleza agizo la serikali, lengo ni kufikisha ekari 200.

Aidha, anasema Taifa haliwezi kuwa na chakula bora bila ya mbegu, hivyo wao JKT wamejikita katika kuzalisha mbegu bora, wakikusudia kila zao linalozalishwa JKT linaenda kuchakatwa na viwanda vyao ili liwe bora.

"Kikosi hiki kilianza Kilimo cha Mkonge baada ya kupata agizo la serikali kupitia Waziri Mkuu alipoenda Tanga katika ziara, ambako alizitaka taasisi za jeshi zijikite katika mazao ya biashara kama mkonge," anaeleza.

Kanali Lushika anadokeza JKT kutekeleza agizo la serikali kwa vitendo ikilima mazao ya mkakati kama vile mkonge, kahawa, korosho na Michikichi.

### MGAMBO JKT

Kaimu Kamanda kikosi 835 JKT Mgambo Meja Raymond Mwanri, anasema walianza kutekeleza agizo la serikali kwa kulima ekari 100 za mkonge mnamo Juni, mwaka huu kwa kuandaa shamba.

Meja Mwanri anasema, kilichofuata wakapandamkonge Septemba mwaka na wanatarajia kuivuna baada ya miaka mitatu ijayo na anafafanua wanatarajia kuongeza upandaji mbegu hivi karibuni, kuhakikisha wanapata mbegu za kutosha.

Hata hivyo, Kamanda hiyo anadokeza kukabiliwa na kikwazo cha wanyama waharibifu kama vile ngedere, nyani na nguruwe.

### MARAMBA JKT

Emmanuel Muluga kutoka JKT Maramba, anasema kambi yake imelima ekari 100 kama za Mgambo, lakini mwakani wanatarajia kuongeza ekari nyingine kuhakikisha wanafikia lengo la kulima ekari 200 kama walivyopanga hapo awali.

"Kwa kweli hakuna kinachoshindikana JKT. Hizi ekari ambazo zimepangwa kulimwa zitalimwa tu na zitastawi kwa sababu zinalimwa kitaalam," anasema Muluga

Anaahidi kuwa mkakati huo utatekelezwa kitaalamu kwa kutumia wajuzi wake wa ndani wa kilimo, akiongeza kuwa lengo kuu walilo nalo ekari hizo za mwanzo zinakuwa shamba darasa kwa jamii, ili wengi wafike kujifunza, zao hili linalovunwa ndani ya miaka 15, ikiwa na faida kubwa kwa mlimaji.

### KIJANA WA KUJITOLEA

Kijana askari wa kujitolea kikosini Mgambo, Hamad Hamisi Shame, anasema:"Tumeweza kujifunza mambo mengi, pia kujua zao la mkonge na maajabu yake,"

Anatanguliza shukrani, kwamba amevuna ujuzi utaomfungulia mlango wa kwenda kujaijiri, baada ya kuhitimu mafunzo, kwani ambako kuna ujuzi huo, pia anafaidika jeshini stadi za nidhamu, kazi na uwajibikaji.

Hivi karibuni, serikali ilitoa agizo la kuwa vikosi vya Jeshi vihakikishe vinaanza kujitegemea na katika moja ya mikakati hiyo, ndio jeshi likabuni miradi kadhaa ya kilimo mkakati na kuanza kulima mazao kadhaa.

Sehemu ya maza hayo ni michikichi, mahindi, maharage, mpunga, mkonge, kahawa, korosho pamoja na shuhuli za uvuvi wa samaki unaofanyika zaidi katikia kikosi cha Chita, mkoani Morogoro.

Kupitia agizo hilo kila kikosi kinalima mazao mbalimbali na hivi sasa jeshi hilo linajitegemea kwa chakula bila bugudha yoyote na moja ya mikakati waliojiwekea ni kuhakikisha jamii inayowazunguka, pia inapata chakula ambacho wanalima katika maeneo ya mashamba yao yanayowazunguka .

Hata hivyo, mkakati huo unaonyesha kufanikiwa kwa kila kikosi kinafanya mkakati chini ya wataalam wa JKT wakishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), ambao wanahusika uendeshaji kilimo hiko katika vikosi vya jeshi hilo.

BIASHARA

# TARI Ukiliguru katika 'amshaamsha' kuirejesha zao kimkakati pamba katika enzi zake kutamba

## • Balozi wake Aggrey Mwanri, awaingiza wadau darasani

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

HADI sasa zaidi ya asilimia 90 ya pamba nchini inalimwa katika eneo la Magharibi kuzunguka Ziwa Victoria. Hata hivyo, kwa miaka kadhaa zao hilo uzalishaji wake umekuwa ukisuasua baada ya soko la dunia kuingia mushkeri.

Sasa katika hilo zama zilizopo serikali ikishikilia bango uzalishaji huo, wataalamu wa kilimo wanahimiza wakulima kujitahidi kupima afya ya udongo kabla hawajaanza kilimo.

Hiyo ina maana kwamba, hapo watatambua kama kuna kasoro kwenye udongo na inapobainika hivyo, mhusika anapewa ushauri wa namna ya kutumia mbolea au virutubisho kuwasaidia.

Dannis Wambura, ni Mtafiti wa Udongo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ukiliguru, anayeeleza umuhimu huo kwa kuchukua sampuli shambani na kuipeleka kwenye taasisi, baadaye wataweza kutambua kasoro kupitia viini tofauti.

Anasema wamejikita katika upimaji vitu vingi vinavyohusina na viini vya udongo na wana vifaa bora vya upimaji, hivyo wakulima watumie fursa hiyo zaidi, kuliko kujikita katika kilimo cha mazoea.

Selesi Mayunga, Ofisa Kilimo na Mtafiti Msaidizi, TARI Ukiriguru, anasema wanafanya uchambuzi wa pamba kwenye majaribio madogo na wana aina tano za mbegu anazozitaja za kiume na sita za kike.

Mayunga anasema, mbegu za kiume wanazioanisha na za kike kupata mbegu chotara na huwa wanafanya, mbegu zenye uvumilivu kiafya, lengo ni kuongeza mavuno.

Anasema mbegu iitwayo 'UkmO8' ipo kwa wakulima na mpaka sasa ndiyo mbegu bora walioanisha kwa ajili ya kuongeza mavuno.

Kwa mujibu wa mtaalamu Mayunga, ekari moja inatoa watani pamba kilo 1000 hadi 1,200 na awali walitumia mbegu aina za 'Uk91' na 'Uk08' ambazo wakulima wanazitumia, lakini uzalishaji wake ulikuwa mdogo.

Anafafanua kwamba wakulima wengi wameenda kujifunza na wamewaelekeza namna ya kuchambua pamba, shida wanayoipata kutoka kwa wakulima ni kulalamikia mbegu ambazo hazioti.

Anaifafanua kwamba, shida kuu ipo kwao na kwa sababu mbegu mama inakuwa na manyoya, baada ya hapo inapelekwa kutoa manyoya ikipelekwa kwa mkulima anayechimba shimo la kupanda.

Mkurugenzi wa Menejimenti ya Maarifa wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Philbert Luhunga, anasema TARI Ukiliguru imetoa mbegu nyingi kulinganisha na za awali, hivyo teknolojia zote hizo zinapaswa ziwafikie wakulima ipasavyo kuongeza tija kwenye uzalishaji.

### BALOZI WA PAMBA

Aggrey Mwanri, ni Balozi wa zao la pamba nchini anayehimiza mkoa huo kuzalisha tani 70,000 za zao hilo, huku kitaifa zikitarajiwa kuzalishwa tani milioni moja.

Mwanri anasema kampeni ya uhamasishaji wa kuongeza tija ya uzalishaji pamba inalenga kuwapa ushauri, utakaowafanya viongozi wachukue uamuzi sahihi kuhusu zao hilo.

Balozi huyo ambaye kabla ya kustaafu hivi karibuni, alikuwa Mkuu wa Mkoa Tabora, anawataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi, wajitahidi kuongeza tija kwenye zao hilo katika jitihada za kufikisha malengo ya kuzalisha tani milioni moja za pamba.

"Rais anazungumza kutupeleka kwenye Uchumi wa Kati. Ni makazi na huwezi akizungumzia mapinduzi ya viwanda bila kuwa na malighafi. Tunataka uwekezaji wa pamba kimkakati ambao utatupa mtaji, ajira na ongezeko la mapato ya serikali," anasema.

Mwanri anafafanua zaidi: "Kazi ya kichwa ni kufikiri, si kubeba mzigo na hakuna mkulima duni asiye na akili, mawazo."

Anaeleza kuwa uzalishaji pamba kwa wakulima nchini uko katika wastani wa kilo 100 hadi 300 kwa ekari na anaoanisha umuhimu wake katika tafsiri ya upungufu, kuna wakati viwanda vinavyohudumia zao hilo vinafungwa kwa miezi kadhaa, kwa kukosa malighafi.

Rai yake ni kwamba viongozi wa kiserikali wawaelimishe wakulima vijijini kwa kuzingatia matumizi ya kanuni bora za kilimo na matumizi ya pembejeo.

### MTAALAMU TARI

Dk. Paul Saidia kutoka TARI, anaeleza kituo hicho kilianza kufanya kazi mwaka 1930, ikiwa sehemu ya shamba la serikali ya mitaa inayozalisha mbegu za pamba na kazi za utafiti zilianzishwa mwaka 1932, msisitizo mkubwa ukiwa zao la pamba.

Anasema jukumu lao kubwa ni kufundisha wakulima: Matumizi bora ya maji; namna ilivyo rutuba ya udongo, tathimini na kuchora ramani yake, sambamba na maabara ya udongo.

Mengine kwa mujibu wa Dk. Saidia, ugunduzi wa mbegu na uzalishaji wake; mbinu bora za uzalishaji; na kutunza mashamba.

Anasema wamejikita katika kudhibiti vinavyowasumbua ambavyo vinajumuisha magonjwa, wadudu, magugu, hali ya hewa na kuongeza thamani ya usindikaji.

"Lengo letu kuu ni kuchangia kuboresha tija ya kilimo kwa kufanya utafiti shirikishi unaozingatia mahitaji ya wadau, kuchangia kuboresha motisha na mazingira ya kufanya kazi na kutoa teknolojia sahihi na zenye ubora," anasisitiza Dk. Saidia.

### UONGOZI WA MKOA

Mkuu wa Mkoa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, anasema wao ni miongoni mwa mikoa inayolima na kuzalisha zao la pamba, hivyo anawataka wakurugenzi wa halmashauri za kila wilaya, wahakikishe maofisa ugani wake wanakuwa na mashamba darasa ya mfano ya kuwafundishia wakulima ili wazalishe shambani; kilo 800 hadi 1000 kwa ekari.

Anasema katika mwaka wa fedha 2016 /17, uzalishaji wa pamba mkoani humo ulikuwa tani 11,531; mwaka 2017/18 zilizalishwa tani 17,376; huku 2018 /19 zikizalishwa tani 33,010; na mwaka 2019 /20 kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, ziliambuliwa tani 8,039.

Anasema pamba ni moja ya vyanzo vya mapato kwa wananchi, mavuno yalipofikia tani 33,010 yaliingiza Sh. bilioni 39.612, hivyo umma unaweza kuzalisha kwa tija ikizingatia namna wataalam hao watakavyotoa ufafanuzi wao wa kinachopaswa kuongezwa.

Anasema ni wakati wa kujifunza kuzalisha kwa tija kwa kuzingatia wataalamu ambaye atasaidia kuelekeza nini kifanyike ili kuongeza uzalishaji.

"Tutahakikisha tunajipanga na wataalamu ili elimu hiyo ifike vijijini ambako kuna wakulima, ili kuwasaidia kutambua nini maana ya matumizi ya vipimo, mbolea, mbegu bora, viuadudu," anaeleza Mhandisi Gabriel.

Mkuu wa Mkoa ana rai kwamba, halmashauri mkoani hapo zitumie asilimia 10 ya ushuru wake kuimarisha ulimaji pamba, akiwahimiza maofisa ugani vijijini kuanzisha mashamba darasa yaliyozingatia kanuni za kilimo wawafundishe wakulima waongeze tija kwenye zao la pamba.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salim Kalli, anataka kulipokea na somo akiwahakikisha analifikisha kwa wananchi, ili kuboresha kilimo hicho kufikia malengo stahiki.

Anasema wakazi wa Magu zaidi ya asilimia 75 ni wakulima na zao kubwa wanalolima ni pamba, balio ndio mkombozi kwa wananchi wa eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya anarejea msimu wa kilimo 2020. 2021 lilikuwapo shamba darasa katika Mkoa wa Mwanza na mtazamo wake ni wakulima wakifuata taratibu zote za kilimo, watapata mazao mengi yenye manufaa kwao.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Magu - Kalli, pamba inawaletea faida, huku katika dira ijayo, wamejipanga kulima hekta 18,912 zenye matarajio ya kutoa tani za pamba 22,974 wakiwa na uhakika na malengo yao, kwa sababu wananchi wao wameelimisha vya ngazi ya juu



Dannis Wambura, Mtafiti wa Udongo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ukiliguru (mwenye shati miraba) akieleza jambo kuhusu upimaji udongo unavyoendeshwa maabara kabla ya kilimo. **PICHA ZOTE: NEEMA EMMANUEL**

> **"Wakazi wa Magu zaidi ya asilimia 75 ni wakulima na zao kubwa wanalolima ni pamba, ambalo ndio mkombozi kwa wananchi wa eneo hilo.**




Pamba iliyooteshwa kwa ajili ya majaribio, baadhi zikiwa na mbegu za kuime na zingine za kike, ili kupata mbegu chotara, katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ukiliguru .

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Nendeni kwa usalama barabarani






**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

MWAKA fulani hivi si zamani sana, katika tembea tembea yangu hivi, nilipata fursa ya kwenda Mashariki ya Mbali, kuna nchi huko inaitwa Korea Kusini.

Nilikuwa jiji linaitwa Seoul, ambao ndio mji mkuu wa nchi hiyo ndugu na Korea Kaskazini ya Kim Jong-un. Ni mji mzuri tu wenye miundombinu mingi mizuri, lakini yenye idadi kubwa ya watu.

Sikushangaa kuona magari mengi barabarani, katika barabara zenye nafasi kubwa ya madereva kutamba, lakini si kushindana kama walivyo wa nchi hizi za kwetu ambao hushindana.

Nilishangaa lakini, kutosikia honi au paipu za magari hasa kutoka na na wingi wa magari lakini na kasi pia. Kushangaa kwangu kukashangaliwa na kiongozi wetu wa msafara, mwenyeji wetu.

Akanipa jibu la mkato tu kuwa hapa 'nchini ukisikika unapiga honi ovyo barabarani ni kesi kubwa, kwa sababu ni kama uchafuzi wa mazingira tu kutokana na kelele. Nilipotoka Korea Kusini katika tembea hiyo, nikajikuta niko Marekani, katika jiji maarufu la Washington, D.C. Hapo nikiwa na mwenyeji wangu, tukafika mahali kwenye mataa ya kuongozea magari barabarani.

Madereva wanaheshimu sana si tu wa magari, lakini hata wa pikipiki, kila anayeona taa nyekundu anasimama kusubiri ya kijani imruhusu. Nikahoji kijinga, mbona hata wa pikipiki wanasimama?

Mwenyeji akaniangalia pia kwa jicho la kijinga, akanihoji ulitarajia wafanye nini? Nikamwambia mbona Bongo hapa bodaboda tusingekuwa tunawaona hapa wangeshapotelea mbele huko.

Akacheka kwa dharau ya kijinga tena, akaniambia hapa bwana hayo mataa yana kamera ndani, ukipita tu baada ya muda mfupi simu yako italia na kukupa ujumbe wa nenda kalipe faini yako ya dola kadhaa.

Sikuwa na swali tena, nikazungumzia mengine yakiwamo ya kunionyesha maduka ambako nitanunua zawadi kwa ajili ya wategemezi waliobaki Bongo. Tukaenda huko, kisha akanishusha hotelini.

Wakati nimejilaza nafikiria safari yangu ya kurudi Bongo na nini nitawambia Wabongo, nikaunganisha nilichokiona Seoul na hiki cha Washington, D.C. Kule hakuna honi, huku mataa yana kamera.

Mawazo nikayarudisha Bongo kwa muda, nikaona jinsi mabodaboda wanavyofanya fujo barabarani. Nikaona jinsi matrafiki wanavyowachekea tu. Wakiwatazama kana kwamba hawawaoni.

Nikalifikiria Bunge lililowapunguzia faini kutoka Sh. 30,000 mpaka Sh. 10,000! Unampunguzia mhalifu adhabu ili aendelee kuhalifu! Si ndiyo maana yake!

Nikaona jinsi bodaboda siku hizi walivyaamua kufunga honi za malori kwenye pikipiki zao, kama uko mbele na gari au baiskeli ukasikia honi ya lori tena nyuma yako bila shaka unaweza kuachia usukani ukagonga au kubamiza kingo za barabara, kama si kuingia mtaroni.

Siku hizi bodaboda zimefunga muziki, wanaita muziki mzito, kelele kama kitu gani sijui. Wanapita humo humo walimosimama matrafiki, hawasimamishi kwa sababu faini ni Sh. 10,000.

Nabaki najiuliza hivi Tanzania tunaenda wapi? Bodaboda ndio wanaotawala miji, kama walivyokuwa wanatawala wamachinga kwenye tasnia ya biashara. Kila kona mmachinga, maduka yakawa hayaonekani.

Leo bodaboda wanatawala njia, wanatawala barabara, wanatawala mpaka sheria za usalama barabarani, wanapita wanakotaka, hawatambui kuna alama za waenda kwa miguu, hawatambui kuna taa za barabarani, hawatambui kuna walemavu wala wagonjwa.

Bila shaka hawa nao wako juu ya sheria za usalama barabarani kama walivyo madereva wa serikali ambako kote wao wanapita tena kwa kasi wanayoikadiria wao na huenda wakigongana na chombo kisicho cha serikali, kosa litakuwa kwa chombo hicho.

Haya sasa, Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani ndiyo hiyo inabisha hodi. Kagueni basi bodaboda hao hasa wenye honi za malori na mabasi, waziondoe. Kagueni redio zinazopiga kelele kwenye bodaboda na bajaji. Nazo ziondolewe.

Tuepuke kuwa na jamii ya kambare, baba sharubu mtoto sharubu, hatutafika, kwa sababu jamii bila utaratibu inakuwa jamii wa wanyama. Kuna sababu gani ya kutoa leseni kwa mtu anayekiuka sheria iliyompa leseni? Alamsiki!

BIASHARA

BAADA KUWEZESHWA NA CHAVITA...

# Kijana athibitisha anaweza; ni seremala kamili, ana familia, nyumba na wapangaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NI mafanikio kwa kijana mwenye ulemavu kiziwi. Abasi Kumpuni (32), mkazi wa Kihonda katika Manispaa ya Morogoro baada ya vita vikubwa vya maisha, sasa ni mtaalam fundi na anaishi kwenye makazi yake, hasumbuliwi na mwenye nyumba.

Kama inavyonenwa 'usione vyaelea vimeundwa.' Ni zao la mkakati wa kipekee wenye mzizi kutoka Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) mkoani Morogoro, mwaka 2000 ikawaundia karakana jirani na ofisi, naye akawa miongoni mwa waliojitosa kuanza kuwajifunza hadi kuwajibika.

Hatua aliyofikia, sasa anajinasibu kitaaluma ni fundi seremala, anayeishi katika makazi yake yenye thamani zaidi ya Sh. milioni 12, akiwa na mkewe, katika nyumba ya vyumba saba akiwa na wapangaji watatu.

Kumpuni anasema, ameanza kuwa na mpango wa kujenga nyumba kuanzia tangu ofisi ya CHAVITA ilipoanzishwa na yeye kuanza kazi hiyo na baada ya miaka mitatu, mwaka 2003 alianza ujenzi uliokamilika mwaka jana.

Mbinu aliyotumia ni kuweka akiba benki kwa hatua na mahitaji mengine amekuwa akitengeneza mwenyewe, kwa kusaidiwa na wenzake kama vile matofali ya kuchoma.

Anasema, akiwa fundi selemara kwenye Mtaa wa Kitope, katika Kata ya Boma, huwa anapata faida wastani kati ya Sh. 100,000 hadi 200, 000 kwa mwezi ambayo kiasi kidogo hulazimika kuweka benki na zingine anaziingiza kwenye mtaji kwa kununua malighafi za ufundi na kutengeneza, kisha anaziweka nje kwa ajili ya kuvutia wateja.

Anasema anatengeneza samani za majumbani aina mbalimbali kama vile vitanda, kabati, meza za ndani na za jikoni, viti vodogo (stuli), makochi na vibao vya kusukumia chapati,

"Mfano nimetengeneza kabati na mtu akalipenda, anaweza akanunua kwa Sh. 150,000 hadi 180,000. Naitenga pesa hiyo katika mahitaji yangu ya kawaida, kuboresha biashara na kidogo naweka benki," anaeleza Kumpuni.

Sasa anawaasa vijana wenzake kujituma kwa kufanya ujasiriamali wa aina mbalimbali, ili kupata pesa za kujikimu kimaisha.

"Mimi kwa sasa napata faida kwenye kazi yangu hii na nyumbani wapangaji wananilipa kwa mwezi napata Sh.75,000. Zinanisaidia kujikimu kwenye maisha yangu, sababu kila chumba mpangaji analipa Sh. 15, 000," anasema.

Anasema, mpango wake ni kukusanya fedha zaidi kwa ajili ya kuboresha nyumba yake na kuongeza malipo ya kodi, ambayo anadai yatamsaidia katika mambo mbalimbali ya maendeleo.



Abasi Kumpuni (32), akiwa katika eneo lake la shughuli za useremala. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

> **"Mimi kwa sasa napata faida kwenye kazi yangu hii na nyumbani wapangaji wananilipa kwa mwezi napata Sh.75,000.**

### MAGUMU JE?

Kumpuni anasema, licha ya mafanikio aliyoyapata, amekuwa akikumbana na changamoto ya kukosa mtaji wa uhakika na kusababisha wakati mwingine anakosa fenicha za kuandaa kuweka kwa ajili ya kuonyesha wateja wapiti njia.

"Wakati mwingine mteja ana nia ya kutengeneza bidhaa kwangu, lakini haniamini kama naweza. Hivyo, ataishia kuondoka nampoteza mteja. Kuweka fenicha niliyotengeneza nje kunanisaidia mteja kusogea na kuweka oda ya kutengenezwa fenicha kama ile au hata nyingine," anasema Kumpuni.

### KATIBU CHAVITA

Katibu wa CHAVITA Mkoa wa Morogoro, Salumu Ally, anasema waliamua kuweka karakana hiyo jirani na ofisi hizo ili kuwasaidia vijana wenye uziwi na usikivu hafifu wajiajiri baada ya kujifunza ufundi seremala, kwa sababu awali waliweka mwalimu na baadae akabakia Kumpuni, ambaye yupo hadi sasa.

"Tulianzisha karakana hii tukiwa hatuna hata kitendea kazi kimoja. Tuliombaomba kwa wadau na hivyo kupata vifaa kama randa na vingine na kutafuta mwalimu wa kuwafundisha vijana wetu na sasa wenyewe ndio wanafundishana," anasema Ally.

Anafafanua tayari wasiosikia tisa waliokuwa wakijifunza kwenye karakana hiyo wanaendeleza shughuli zao baada ya kupata mafanikio na mitaji.

Anafafanua kuwa wawili kutuma timu ya viziwi tisa waliofanya shughuli za useremala eneo la 77 Morogoro, kwa sasa wawili jijini Mwanza wamefungua maduka ya vipodozi na watano wapo Morogoro na Mbeya, wakifanya shughuli za uinjilishaji wa neno la Mungu katika Kanisa dogo la Emmanuel, lililo chini ya Kanisa la Anglikana.

Katibu huyio anasema, licha ya kupata mafanikio hayo bado wanakabiliwa na shida ya kuwapo vijana wanaokaa majumbani mwao bila ta kujishughulisha na masuala ya kukuza uchumi.

Anasema wapo wanawake wanaobanwa na wazazi wao, ambao hawataki kuwaacha watoke sehemu moja hadi kwingine kujitafutia riziki, sasa anawashauri wazazi wa wasichana wasiosikia kuwapa nafasi watoto wao, ili waonyeshe uwezo wao wa kufanya wanavyoweza katika shughuli za kukuza uchumi.

### NENO LA MTEJA

Mmoja wa wateja wa aliyekutwa akinunua bidhaa dukani kwa Kumpuni, Alex Kipanti, mkazi wa Manispaa ya Morogoro, anasema watu wenye ulemavu wanapaswa kupewa 'sapoti' kwa mambo ya maendeleo wanayofanya.

Kipanti anasema, jamii inapaswa kutambua kuwa kwa kuvipa kipaumbele vitu wanavyotengeneza na kutowachukulia kwamba hawawezi kutengeneza vitu vizuri.

"Nilipita nikakuta anatengeneza bidhaa hapa, nami nikavutiwa nikaoda kutengenezewa kabati la vitabu, akasema anataka nilipie Sh. 120,000 na ndio nimekuja kulifuata, ni zuri!" anasema Kipanti.

Mjasiriamali asiyesikia kama alivyo Kipanti, Nzile Ayubu (36), anayepatikana eneo la sabasaba, anawaasa wasiosikia viziwi wenzake kutambua kwamba, kukaa bila kazi au biashara hakutawasaidia katika maisha yao.

Anasema, suala la wao kukaa bila kazi haliwezekani kwani wanapaswa kufanya kazi ili kujisaidia na kusaidia familia zao ikiwemo watoto wao.

"Hata na kwa wasiokuwa na familia wanapaswa kujituma na kujiajiri na sio kutegemea kuajiriwa, waingize kipato cha kusukuma maisha yao na kujisaidia hata watakapokuwa na maisha yao baadae wasiyumbe," anasema Ayubu.

Chama cha Viziwi Mkoa wa Morogoro, kina jumla ya wanachama 250, wakijumuishwa na watu wazima, wanafunzi wanaosoma shule maalum za msingi na sekondari na watoto wasioanza shule.



## HABARI DODOMA

# Mawaziri wakutana kujadili mpango lishe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAWAZIRI wa sekta zinazotekeleza mpango wa lishe wamekutana jijini hapa kwa lengo la kujadili na kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu maandalizi ya mkutano wa mwaka wa wadau wa lishe utakaofanyika mkoani Tanga Novemba 17, mwaka huu.

Akizungumza juzi wakati wa mkutano huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema wameandaa mkutano huo kwa kushirikiana na wizara zinazotekeleza mpango wa lishe.

"Pamoja na wadau wa lishe kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa masuala ya lishe pamoja na mikakati ya serikali katika kupunguza utapiamlo nchini, suala la lishe ni mtambuka linalosimamiwa kwa ujumla wetu mkitizama sekta ambazo zipo hapa zinaguswa moja kwa moja kwenye suala hili la lishe bora na kupambana na udumavu, utapiamlo na mambo mengine yanayohusu lishe," alisema.

Waziri Mhagama alisema Ofisi ya Waziri Mkuu katika kufanikisha hayo, imekamilisha maandalizi ya mpango jumuishi wa kitaifa wa pili wa masuala ya lishe (2020/21-2025/26) ambao utatoa mwongozo wa utekelezaji wa afua za lishe hapa nchini kwa miaka mitano.

Mhagama aliongeza kuwa Mkutano huo wa mwaka utafanyika mkoani Tanga kwa lengo la kuhamasisha wananchi wa mkoa huo kuongeza jitihada katika masuala ya lishe na hivyo kurudisha mkoa huo katika nafasi iliyokuwa awali na ikiwezekana kufanya vizuri zaidi.

"Zamani mkoa wa Tanga ulikuwa unafanya vizuri kwenye masula ya lishe lakini hivi karibuni umeonekana kuwa na kiwango cha udumavu katika masuala ya lishe, hivyo unahitaji uhamasishaji wa hali ya juu katika masuala ya lishe ili kuwa moja ya mikoa itakuwa kielelezo cha mafaniko katika utekelezaji wa mpango jumuishi wa kitaifa wa pili wa masuala ya lishe," alisema.

Mhagama alipongeza juhudi zilizochukuliwa katika kusimamia mapambano dhidi ya utapiamlo ambapo alieleza jitihada hizo za wazi zitawezesha kufikia malengo waliyojiwekea katika kupunguza viwango vya utapiamlo nchini.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Prof. Jamal Katundu, alisema Tanzania ni nchi mwanachama wa Vuguvugu la Lishe Duniani na kama taifa walipokea mwaliko wa kushiriki katika mkutano huo wa wadau wa lishe wa mwaka 2021 unaojulikana kama Nutrition for Growth Summit (N4G) utakaofanyika kwa njia ya mtandao Desemba 7 na 8, mwaka huu, Tokyo nchini Japan.

# Sheria kuwabana wasiorejesha mikopo halmashauri sasa yaiva

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema anakusudia kupeleka muswada wa sheria bungeni ili kuwabana wanaokopa na kushindwa kurejesha kwa wakati mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini.

Pia amesema anakusudia kuandaa hoja nyingine ya kupeleka bungeni ya kupunguza idadi ya watu kwenye vikundi ambayo inatumika hivi sasa ya watu watano hadi watatu.

Alisema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akikabidhi mfano wa hundi ya mikopo kwa vikundi 48 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hafla iliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square.

Ummy alisema kuwa kutokana na wakopaji walio wengi kutokuwa waaminifu katika kurudisha mikopo kwa wakati inawanyima fursa watu wengine kukopa fedha hizo zinazotolewa na halmashauri.

"Ninakusudia kupeleka muswada bungeni huo kwa ajili ya kuwabana wanaopewa mikopo hiyo na hawataki kurudisha na wengine kuamua kutoroka nayo.

"Suala hili nitalipeleka bungeni kwa ajili ya kupendekeza sheria itakayowabana wanaokopa mikopo hiyo ili waweze kulipa tofauti na sasa watu wamekuwa wakitoroka na fedha na kuingizia serikali hasara kubwa ya mamilioni," alisema.

Pia alisema pendekezo lingine ni kupunguza idadi ya watu kwenye vikundi kutoka watano hadi watatu ili kuwapatia mikopo yenye tija ili warudishe kwa wakati.

Waziri Ummy aliwataka wakopaji wa fedha hizo hususani vijana kurudisha mikopo hiyo kwa wakati kwa kuwa wameonekana kuwa sugu katika kurudisha.

Alisema vijana wamekuwa sugu wa kutorudisha mikopo tofauti na wengine kama vile vikundi vya watu wenye ulemavu na wanawake.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akizungumza kwenye hafla hiyo, alisema jumla ya Sh. bilioni 1.39 zimetolewa kwa vikundi 48. Alitaja kiasi na vikundi kwenye mabano kuwa ni wanawake (Sh. milioni 524), vijana (Sh. milioni 463.35) na watu wenye ulemavu Sh. milioni 51.7.




Mwakilishi wa Balozi wa Norway hapa nchini, Karen Asla, akizungumza katika uzinduzi wa mafunzo ya programu ya mwanamke kiongozi kwa wabunge wanawake yaliyoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), kwenye Ukumbi wa Msekwa, jijini Dodoma juzi.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ziwa Victoria kumaliza kero ya maji Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema maji ya Ziwa Victoria ndiyo yanaweza kuwa suluhisho pekee la kukomesha tatizo la huduma hiyo katika jiji la Dodoma.

Aweso alibainisha hayo jijini Dodoma juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya maji katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Waziri alisema suluhu pekee ya uhaba wa maji katika jiji la Dodoma ni maji kutoka katika ziwa hilo na si vinginevyo.

Kutokana na serikali kuhamishia makao makuu Dodoma, alisema kumekuwa na uhitaji mkubwa wa maji kulinganisha na kipindi cha nyuma.

Pamoja na kuwapo kwa jitihada mbalimbali za kulifanyia kazi tatizo hilo katika jiji la Dodoma, alisema bado kuna haja ya kutoa maji Ziwa Victoria ili kukomesha moja kwa moja kero hiyo.

"Maji ya Ziwa Victoria tayari serikali ilishapeleka katika miji ya Kahama na Shinyanga lakini pia hivi sasa Rais Samia (Suluhu Hassan) ametuagiza kuhahakisha yanafika katika jiji la Dodoma ili kuondoa kabisa kero ya maji katika makao makuu ya nchi," alisema Aweso.

Pia alisema katika kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi, wizara imepanga kujenga mabwawa makubwa ya Farkwa, Kidunda, Songwe na Ndembera/Lugoda na mabwawa ya ukubwa wa kati katika sehemu mbalimbali nchini.

Vilevile alisema serikali imepanga kutekeleza miradi itakayotumia vyanzo vya maji vya uhakika vikiwamo maziwa makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria na mito mikubwa kama Mto Ruvuma, Rufiji, Kiwira, Songwe na Kagera.

Alisema miradi hiyo itahusisha ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kutoka maeneo yenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba.



# RC aagiza hati za wafanyakazi wa kigeni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza Idara ya Uhamiaji mkoani hapa kushikilia hati za kusafiria za wafanyakazi tisa wa mkandarasi aliyepewa kazi ya kuunganisha mitambo katika kiwanda cha kuzalisha bidhaa zitokanazo na mahindi cha East Africa Starch mpaka watakapomaliza kazi hiyo.

Wafanyakazi hao ni wa Kampuni ya Sarfraz Ladhani Raj Processing yenye asili ya India ambao wanadaiwa kuchelewa kukamilisha kazi hiyo huku wakitaka kutoroka kabla ya kukamilisha jukumu hilo.

Kiwanda hicho kinatokana na kubadili matumizi ya kilichokuwa kiwanda cha kutengeneza nguo cha Mbeya Textile kilichoko eneo la Songwe Viwandani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Homera alitoa agizo hilo wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipofanya ziara katika kiwanda hicho kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi kutokana na kuchukua muda mrefu bila kukamilika.

Akiwa katika eneo hilo, Homera alielezwa na uongozi wa kiwanda hicho kwamba wafanyakazi wa kampuni hiyo licha ya kulipwa fedha zao zote wamekuwa wakisuasua kufanya kazi hali ambayo inawasababishia hasara.

Ofisa Utumishi wa Kiwanda hicho, Mariam Bakari, alisema kiwanda hicho kilibadilishwa matumizi kutoka kutengeneza nguo na kutengeneza bidhaa zitokanazo na mahindi baada ya kuadimika kwa pamba katika eneo hilo.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho kipya ulianza mwaka 2017 na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2019 lakini mpaka sasa bado haujakamilika kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wafanyakazi wa mkandarasi kutaka kutoroka kurudi India.

"Vitendo vya wafanyakazi hawa kutaka kuondoka wakati hawajamaliza kazi na kukabidhi kimekuwa kikitukwaza. Tumehangaika kwenye mamlaka mbalimbali ikiwamo Ubalozi wa India nchini pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje (na Ushirikiano wa Afrika Mashariki) lakini bado hatujapata suluhu ya kudumu," alisema Bakari.

Alisema kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa kinazalisha wanga, chakula cha mifugo na mafuta ya kupikia yatokanayo na mahindi, hivyo akaiomba serikali iwasaidie kutoa msukumo kwa mkandarasi.

Mwakilishi wa Kampuni ya Export Trading ambao ni wabia katika kiwanda hicho, James Maliki, alisema kiwanda hicho kitakuwa na manufaa ya kiuchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Mbeya na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema kiwanda kitasaidia wakulima kupata soko la moja kwa moja la mahindi pamoja na kuajiri watu 3,000 mpaka 6,000 ambao watakuwa wanafanya kazi katika idara mbalimbali.

"Kiwanda kitaanza uzalishaji kwa kutumia tani 45,000 za mahindi lakini lengo ni kufikia tani 90,000 ambazo tutakuwa tunanunua kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Tunaiomba serikali itusaidie maana wanapochelewa wanatutengenezea hasara," alisema Maliki.

Baada ya maelezo hayo, homera alimwagiza Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Kigongo Shikille, kuzishikilia hati hizo huku akiwataka wafanyakazi hao kukamilisha kazi ya kufunga mitambo ndani ya siku 10.

Alisema mpaka watakapokamilisha kazi hiyo na mitambo kufanyiwa majaribio, ndipo watarejeshewa hati zao na wawe na uhuru wa kurejea kwao.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Chande akizungumza wakati akifungua mradi wa urejeshwaji endelevu wa mazingira na hifadhi ya Bioanuai Tanzania, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# LATRA yataja kiini ajali barabarani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Tanzania (LATRA) imesema ajali nyingi zimekuwa zikitokea mkoani Mbeya na kugharimu maisha ya watu kutokana na ubovu wa vyombo vya usafiri vinavyotumika mkoani humo.

Pia mamlaka hiyo imesema katikati ya Jiji la Mbeya, kumekuwa kukitokea ajali na migogoro ya wasafirishaji kutokana na mwingiliano wa vyombo vikubwa na vidogo vya usafiri na usafirishaji.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa mkutano wa wadau mbalimbali wa usafirishaji uliokuwa umelenga kutoa elimu kuhusu Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani.

Wadau walioshiriki kwenye mkutano huo ni Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wamiliki wa vyombo vya usafiri vya ndani ya mkoa wa Mbeya na wa masafa marefu, watetezi wa abiria, wawakilishi wa vyama vya madereva na makondakta na mabalozi wa usalama barabarani.

Ngewe alisema kutokana na tatizo hilo, waliamua kutoa elimu kwa makundi yote ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea pamoja na vurugu ambazo zimekuwa zikisababishwa na mwingiliano wa vyombo vya usafiri.

"Tunashauri wasafirishaji wetu waungane kwenye vikundi ili wawe na uwezo wa kununua vyombo vya usafiri vyenye ubora ambavyo vitawasafirisha watu kutoka majumbani kwenda kazini na kurudi wakiwa salama," alisema Ngewe.

Alisema Mbeya ni moja ya mikoa ambayo ina shughuli nyingi za kufanya, hivyo kinachotakiwa ni wananchi kuwa na uhakika wa kusafiri kwenda kwenye shughuli zao na kurudi wakiwa salama.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwapongeza wadau wa usafirishaji katika mkoa huo kwa kufanya kazi kubwa ya kupunguza tatizo la ajali za barabarani kwa kutoa elimu ya usalama barabarani.

Homera alisema kwa sasa ajali katika mkoa zimepungua kwa zaidi ya asilimia tano jambo ambalo alisema linatia matumaini ya kumaliza kabisa ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu na kuwaacha wengine na ulemavu.

Alisema serikali inaendelea na mipango ya kumaliza ajali ukiwamo mpango wa upanuzi wa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kutoka Igawa wilayani Mbarali mpaka Tunduma mkoani Songwe.

# UWT yasaka mil. 78/- ujenzi ofisi na nyumba

**Na Nebart Msokwa** MBARALI

UMOJA wa Wanawake wa Tanzania (UWT) Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, unahitaji zaidi ya Sh. milioni 78 kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi, nyumba ya mtumishi na vifaa vya ofisini.

Katibu wa UWT Wilaya ya Mbarali, Suzan Mheza, aliyasema hayo wakati wa kikao cha wajumbe wa umoja huo kilichoitishwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, ambaye alikuwa na ziara ya kutembelea jumuiya hiyo.

Alisema umoja huo umekuwa ukikabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kukosa vitegauchumi jambo ambalo linawalazimu kuanza kuchangishana wanapotaka kufanya jambo lolote ikiwamo kupokea wageni.

Alisema kwa sasa wanachotaka ni kuwa na kitegauchumi ambacho kitakuwa chanzo cha uhakika cha mapato kitakachousaidia umoja huo kujiendesha.

"Tunahitaji fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza mradi wetu, kwa sasa mradi huu upo kwenye hatua za awali hivyo tunaomba tuungwe mkono ili tufanikishe mradi wetu na tuwe na uwezo wa kuinuana kiuchumi," alisema Suzan.

Mbunge Fyandomo aliahidi kuupatia umoja huo mashine ya kukoboa, kusaga na kusindika unga wa sembe ili kuongeza kitegauchumi kwa UWT.

Alisema lengo ni kuusaidia umoja huo kutimiza ndoto zake za kuwa na vitega uchumi kwa ajili ya maisha yao pamoja na wategemezi wao wakiwemo watoto.

Pia aliahidi kuwakatia bima za afya wanachama wa umoja huo ili wawe na uhakika wa afya zao huku pia akiahidi kuunganisha Umoja huo na Taasisi mbalimbali ili wapate zabuni za kusambaza unga wakati kiwanda kitakapoanza kufanya kazi.



## Kesi 49 ujauzito zaripotiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya kesi 49 za wanafunzi waliopata ujauzito zimeripotiwa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na wanafunzi 30 wamerejea shuleni kuendelea na masomo.

Hayo yalisemwa juzi na Mrajis wa Elimu, Zuwena Mataka Hafidh, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa utoaji wa taarifa za mwaka mmoja za uongozi wa Rais Dk. Hussein Mwinyi kupitia Wizara ya Elimu mjini hapa.

Alisema kati ya wanafunzi hao 49 waliopata ujauzito, 25 ni kwa shule za Unguja na 24 kwa shule za Pemba.

"Ofisi ya Mrajis wa Elimu inaendelea kufuatilia kesi za ujauzito wa wanafunzi ambao wanasoma katika ngazi ya elimu ya lazima na kuwarejesha shuleni baada ya kujifungua kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya mwaka 2005 ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja," alisema Mrajis.

Alisema kati ya kesi hizo 49, wilaya ya Kusini Unguja inaongoza kwa kuwa na kesi 11, wilaya ya Mkoani Pemba kesi saba, Chakechake kesi sita, Micheweni Pemba kesi sita, Wilaya ya Wete Pemba kesi tano, Kaskazini B Unguja kesi nne, Kaskazini A kesi tatu, Wilaya ya Kati kesi nne na Wilaya ya Mjini Magharibi A na Magharib B kesi moja kwa kila wilaya.

Kuhusu usajili wa shule za serikali, binafsi na vyuo vya elimu kwa muda wa mwaka mmoja uliopita, mrajis huyo alisema shule 38 za serikali zimepatiwa usajili na shule binafsi 72.

Pia alisema vyuo viwili vya binafsi vya ualimu vimesajiliwa kutoa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti na stashahada ya ualimu wa maandalizi. Alivitaja vyuo hivyo ni Dunga Development College na Samail College cha Gombani, Pemba.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja ofisi yake imefuatilia masuala mbalimbali na kuimarisha baadhi ya huduma ikiwamo uendeshaji wa utoaji wa leseni za kielektroniki kwa walimu.

Sambamba na hilo, alisema wameongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kufuatia mwitiko mzuri wa shule binafsi.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema sekta ya elimu ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya sekta zote, hivyo wizara inatarajia kujenga madarasa 1,131 ili kutoa nafasi mpya kwa wanafunzi 50,895.

# Othman Masoud asisitiza mabadiliko sera ya mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Serikali ya Zanzibar iko tayari kushirikiana na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), kuifanyia mapitio Sera ya Maendeleo ya Mtoto Zanzibar ili kwenda sambamba na mwelekeo wa uhitaji wa serikali.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake, Migombani mjini Zanzibar, alipozungumza na Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF nchini, Laxmi Bhawani.

Alisema kutokana na mambo mbalimbali yanayojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo hivi sasa, inahitaji kufanyiwa mapitio sambamba na kusaidia mpango wa kuimarisha lishe ya mtoto katika kujenga mustakbali bora wa maendeleo ya mtoto wa Zanzibar.

Shirika hilo kwa muda mrefu, alisema limekuwa na mchango mkubwa kuisaidia Zanzibar katika masuala mbalimbali ya maendeleo ya mtoto hasa wenye uhitaji maalum na lishe. Alisema hayo yamepewa umuhimu mkubwa katika kujenga maendeleo ya mtoto Zanzibar.

Othman alisema katika majadiliano hayo pamoja na mambo mengine, wamekubaliana kushirikiana katika kustawisha uhitaji mbalimbali ya watoto wenye mahitaji maalum Zanzibar hasa katika maeneo ambayo yanayonekana kuwa na matatizo zaidi katika ustawi na maendeleo ya mtoto. Kwa mujibu wa Othman, watoto wenye mahitaji maalum yanahjitajika hasa katika maeneo kama ya Micheweni ambayo yanaonekana yako nyuma kwa kuwapo matatizo mengi zaidi yanayoathiri maendeleo ya mtoto katika ukuaji na uimarishaji wa mfumo wa lishe yatapewa kipaumbele.

Alisema alisema katika jitihada hizo za pamoja pia ushirikiano utaelekezwa katika utoaji wa elimu inayohusu mazingira, maendeleo ya mtoto pamoja na lishe bora ili kuwajenga watoto kukua vyema kimwili na kiakili kwa maendeleo ya taifa. Kwa upande wake, Bhawani alisema shirika hilo liko tayari kushirikiana na serikali ya Zanzibar katika kusaidia mambo mbalimbali kwa maendeleo ya mtoto na Zanzibar kwa jumla.

Alisema pia shirika litaimarisha ushirikiano wa wadau na jamii katika kukuuza upatikanaji wa lishe bora kwa watoto sambamba na kutoa elimu kujenga mwamko wa jamii kwa matumizi sahihi ya chakula chenye kujenga liche bora kwa watoto.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud, akikabidhiwa kitabu kinachohusu masuala ya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto Zanzibar na Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia watoto (UNICEF), Laxmi Bhawani, aliyefika ofisini kwake Migombani, Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Apigia debe wanafunzi kusoma sayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Chama cha Wasanifu na Wakadiriaji Majengo Tanzania, Bernad Ndakidemi, alisema wakati umefika kwa wanafunzi wa Tanzania kusoma masomo ya sayansi ili kuwa wahandisi wazuri hapo baadaye.

Amesema hivi sasa makandarasi wengi wamekuwa wakijiajiri kutokana na uwezo walio nao na si kusubiri ajira kutoka serikalini.

Ndakidemi alisema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa sayansi wa Shule ya Sekondari Kiembesamaki, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema msingi wa mafunzo ya sayansi ni kuanza kusoma mapema na kujitahidi katika masomo hayo bila ya kuyadharau. Hivi sasa, alisema, Tanzania imekuwa na wahandisi wazuri wanotoka katika vyuo hasa wale wa fani ya makadiriaji wa majengo.

Alisema katika kufikia malengo kwa vijana lazima kuwe na utayari wa kusoma kwa bidii masomo ya sayansi hasa hisabati kwa vile ndiyo msingi wa masomo ya fani hiyo na kwamba kwa sasa wahandisi wamekuwa watu muhimu katika fani hiyo ambapo kunawatengeza barabara na wajenzi wa magorofa mazuri.

Naye Katibu mkuu wa chama hicho Said Mrisho, alisema fani ya sayansi kwa ulimwengu huu imeonekana kuwa ya umuhimu mkubwa kulingana na fani nyingine .

Alisema kawaida ya wanafunzi wanapomaliza masomo yao hawawezi kujituma na badala yake wakisubiri ajira kutoka katika serikali wakati jambo hilo si sahihi.

Mwanafunzi wa Shule hiyo, Asha Halfani Ali, alisema licha ya kuwa wanafunzi wengi kupenda masomo ya sayansi bado kuna vikwazo vya miundombinu ya vitendea kazi.

"Fani hii ya uhandisi inatupa matumaini makubwa lakini kinachotuvunja moyo mwanafunzi anapomaliza masomo yake ya elimu ya juu na kwenda kuomba nafasi ya ajira, anaambiwa hana uzoefu wa kazi. Uzoefu huo anaupata wapi wakati ndo ametoka chuoni?" alihoji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Goodluck Elibariki Nnko** amepoteza cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya Sekondari Makumira mwaka 2003. Index Number ni **0329/0073.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi ni Kumb namba **ARU/ARU/RB/522227/2021.**

116566602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAIKA JUSTO KISANGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.976 DGY** AINA YA **TOYOTA VITZ** RANGI YA BLUE.CHASSIS NAMBA **SCP105020935.** ENGINE NAMBA **1SZ3012958.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/537818/2021.**

116565902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO**

**Kituo cha CHAMWINO IKULU Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na.58/2021**

**Jina la Mdai.......................................HERMAN MREMA**

**Jina la Mdaiwa.................................JOSEPHA BALLI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Mdai katika Mahakama ya Mwanzo)**

**KWA: JOSEPHA BALLI**

**Kwa kuwa Mdai amelet madai yake kwamba**
**KUJA KUJIBU MADAI YA TALAKA**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15/11/2021 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinanyohusu shauri hili kwa ajili ya kujijitetea.

**ANGALIZO** kama hautohudhiria siku iliyotajwa hapo juu ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 0

HAKIMU

116566102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**

**Mkoa wa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 06/2021**

**Fatma Adam Msigwa............................Marehemu**

**Nuhu Erasto Mnengelwa.....................Mwombaji**

**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa watu wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi. Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 17th ya mwezi wa Desemba, Mwaka 2021.

Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 09th Novemba, Mwaka 2021.

...........................
**HAKIMU MKAZI**

116566202

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP JUDICIAL CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 130 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MARTIN KALIHOSE MWANDA**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by ABDUL ATHUMAN HIMBA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 24th of November, 2021.

Dated at Dar es salaam this 8th day of November, 2021.

Registrar/Senior Resident Magistrate

116566502

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY**

**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**Probate and Administration Cause No. 29 of 2021**

**In the matter of the estate of the late TUMAINI KAKUYU MLEWA**
**Of Kikuyu within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by ISAAC MOHAMED BIRA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of November, 2021.

Dated at DAR ES SALAAM this 10th day of November, 2021.

DEPUTY REGISTRAR

116566702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**

**Mkoa wa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 49/2021**

**Benward Aidan Chatanda...........................Marehemu**

**Veronica Joseph Wella.....................Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANGAZO LA MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi. Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 19th ya mwezi wa Desemba, Mwaka 2021.

Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 11th Novemba, Mwaka 2021.

...........................
**HAKIMU MKAZI**

116566802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE PAUL LAWUO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 934 AVP – MITSUBISH CANTER.** Chassis namba **FE668EV530099.** Engine namba **4D35F19095.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/538234/2021.**

116566902

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**EMANUEL MARCEL TEMU** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili **MC 157 BCT.** Aina yake **FEKONI.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **KIL/MOS/RB/438526/2021.**

116567402

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Ripoti: 7,500 waliuawa DRC muongo mmoja

**Kinshasa,** DRC

WATU 7,500 waliuawa kati ya mwaka 2008 na 2021, wakati wa mashambulizi yapatayo 2,237 kwenye maeneo 700 katika wilaya ya Beni, Kivu Kaskazini na Irumu, Mkoa wa Ituri.

Ripoti ya uchunguzi iliyochapishwa juzi mjini Kinshasa kwa vyombo vya habari, ulibainisha.

Ripoti hiyo ina kichwa cha habari 'Ripoti ya Yotama kuhusu Mauaji ya Beni na Irumu, Ugaidi, Jihadi au Mauaji ya Kimbari ya Nande?'

Utafiti huo ulifanywa na mbunge Tembos Yotama na mbunge wa mkoa Benze Yotama. Katika ripoti yao ya zaidi ya kurasa 800, viongozi hao wawili waliochaguliwa katika wilaya ya Butembo, walisema wametoa wito kwa dhamiri ya kitaifa kutokana na mauaji hayo ya kimbari.

**Ikiwa watu kutoka jamii ya Nande wanalengwa, ni kwa sababu wamepinga kwa muda mrefu utumiaji wa nchi yetu wa vitendo vya ukatili.**

"Hii ni hali ngumu na ya janga, wauaji halisi hawajatambuliwa," alisema mbunge wa kitaifa, Tembos Yotama.

"Ni matukio ya kushangaza kabisa, mashambulizi yanafanywa katika maeneo yenye wanajeshi kupita kiasi na hata serikali hadi sasa inawahusisha waasi wa ADF na mauaji hayo. Maana yake, hata serikali haina uwezo wa kutupa utambulisho wa wazi wa wauaji."

Katika utafiti huo, wabunge wawili kutoka mkoa wa Kivu Kaskazini walisema kuwa kabila moja limelengwa kwa asilimia 95.

"Ikiwa watu kutoka jamii ya Nande wanalengwa, ni kwa sababu wamepinga kwa muda mrefu utumiaji wa nchi yetu wa vitendo vya ukatili," walidai wabunge hao.

Walipendekeza kwamba serikali iandae mikakati mipya ya kukomesha ukatili huo ili kukomesha ukatili.

Wabunge hao wawili wanapendekeza kwa serikali kupitia upya, kurekebisha mkakati huo, kwa sababu mauaji ya watu wengi yameongezeka na kwamba haifai kwa usalama wa Mashariki.

Walipendekeza kwa jumuiya ya kimataifa kuundwa kwa mahakama ya kimataifa ya uhalifu kwa ajili ya DRC na kuanzishwa kwa uchunguzi huru wa kimataifa, kubaini wauaji halisi, ili wafikishwe mahakamani na kwamba haki itendeke katika hali sawa. "

Utafiti huu ulifanyika kwa ushirikiano na Taasisi ya Wakili Mbenze Yotama na kituo cha kukuza demokrasia, sheria na maendeleo. **RFI**



Watu wakikatiza kwenye maji yaliyofurika kutokana na mafuriko ufukweni mwa bahari, eneo la Chennai, nchini India, juzi. Mvua hizo zilinyesha Kusini mwa India na Sri Lanka na kuua takribani watu 40 huku mamlaka za hali ya hewa zikitabiri mvua zaidi siku cha zijazo. **PICHA: REUTERS**

## Boeing kuzifidia familia ajali ya ndege Ethiopia

**Chicago,** MAREKANI

BOEING imefikia makubaliano na familia za watu waliopoteza wapendwa wao 157 katika ajali ya ndege ya Ethiopia 737 Max, iliyopata ajali mwaka 2019.

Watengenezaji wa ndege wamekubali kuwajibika kutokea kwa vifo hivyo kwa mujibu wa mahakama huko Chicago.

Familia zilizopoteza ndugu zao hazitatafuta fidia za kile walichopoteza kutoka kwa kampuni.

Mawakili wa familia zilizoathirika wanasema Boeing bado itawajibishwa kikamilifu, wakikaribisha makubaliano hayo kama hatua muhimu.

Makubaliano yanatoa fursa kwa familia zilizo nje ya Marekani kama vile Ethiopia na Kenya, kudai fidia kupitia mahakama ya Marekani kuliko kwenye mataifa yao jambo ambalo litakuwa gumu na matokeo ya malipo kuwa kidogo.

Mark Pegram kutoka Uingereza ambaye mtoto wake alikuwa mwathirika wa ajali hiyo alisema: Jambo muhimu kwao ni Boeing kukiri kuhusika na kuanguka kwa ndege hiyo na sio kuweka lawama kwa marubani wa Ethiopian Airlines … tulitaka wajisalimishe."

Mama yake Sam Debbie aliiambia BBC: "Tunachoangalia kukifanyia katika fidia yoyote itakayotolewa ni kuanzisha shirika la kusaidia wahitaji kwa jina la Sam. Na hicho ndicho Sam angetaka tufanye."

Ajali mbili mbaya zilizotokea ndani ya miezi mitano ya ndege ya Ethiopia iliyotokea Addis Ababa na kabla ya hapo ajali ya ndege ya Lion Air iliyoanguka baharini karibu na Indonesia, iliashiria kuwa na hitilafu kubwa kwenye ndege.

Ndege hizo zilizuiwa kwa muda wa miezi 20, huku uchunguzi ukiendelea, zimeruhusiwa kurejea kazini baada ya kampuni hiyo kufanya mabadiliko makubwa kwenye programu na mafunzo yao. **BBC**

# China, Marekani kudhibiti mabadiliko tabianchi

**Glasgow,** SCOTLAND

MATAIFA mawili yanayoongoza kwa kuzalisha gesi chafu duniani, China na Marekani, yamekubaliana kuongeza ushirikiano na kuchukua hatua zaidi katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Hatua hiyo inaashiria kuwa mataifa hayo mawili yako tayari kuweka tofauti zao kando na kushirikiana kushughulikia tatizo la ongezeko la joto duniani.

Mjumbe wa China Xie Zhenhua na mwenziwe wa Marekani John Kerry, walisema mataifa hayo mawili yatashirikiana kupunguza uzalishaji wa gesi chafu kwa viwango vilivyoridhiwa kwenye mkutano wa Paris wa mwaka 2015 wa mabadiliko ya tabianchi.

Wajumbe hao walitangaza taarifa hiyo katika mikutano miwili tofauti na waandishi habari, iliyofanyika mjini Glasgow pembezoni mwa mkutano wa COP26.

Xie alisema kutolewa kwa tamko hilo la pamoja kunaonyesha kwamba ushirikiano ni njia pekee kwa China na Marekani, kuonyesha uwajibikaji kwenye suala la uchafuzi wa tabaka la hewa.

"Kwa kufanya kazi pamoja, Marekani na China zinaweza kufikia malengo mengi muhimu yenye manufaa si tu kwa nchi zetu mbili, bali kwa dunia nzima, kama mataifa mawili makubwa duniani, China na Marekani zina wajibu maalum wa kimataifa," alisema Xie Zhenhua.

John Kerry wa Marekani, alisema makubaliano hayo ya ushirikiano yalianza kujadiliwa tangu mwanzoni mwa mwaka jana kati ya marais wa mataifa hayo mawili.

"Naamini licha ya tofauti zetu tulizonazo ni muhimu sana kwetu kuzingatia machafuko. Hili ni janga la uchafuzi wa hali ya hewa. Na ni mojawapo ya matatizo makubwa tunayokabiliana nayo duniani. Na nadhani ni jukumu letu kuchukua uamuzi huu," alisema Kerry.

Serikali zilikubaliana mjini Paris kupunguza kwa uzalishaji wa gesi chafu ili kuhakikisha joto haliongezeki kwa zaidi ya nyuzi joto mbili dunani kote, na kiwango kilicho bora ni kuhakikihsa joto halipandi kwa zaidi ya nyuzi joto 1.5.

Xie alisema, pande zote mbili zinatambua kuwa kuna pengo kati ya juhudi zilizochukuliwa duniani kote kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa na malengo ya mkataba wa Paris, hivyo ushirikiano wao utasaidia kuziba pengo hilo.

Tamko la pamoja limetolewa siku chache baada ya Rais wa Marekani Joe Biden, kuwalaumu marais wa China Xi Jinping na Urusi Vladimir Putin kwa kushindwa kuhudhuria mkutano huo wa COP26.

Aidha, taarifa hiyo imesema kuwa Marekani na China zitaunda timu ambayo itakuwa ikikutana mara kwa mara kujadili hatua za kuchukua kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa. **DW**

HABARI MICHEZO

# UFUKWENI KAMILI KUCHUANA MICHUANO YA COSAFA 2021

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni kinatarajiwa kuondoka nchini Jumatatu kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mashindano ya COSAFA yatakayofanyika kuanzia Novemba 16, mwaka huu nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaama jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa, alisema kikosi chake kitaondoka na wachezaji 14 ambao walionyesha kiwango kizuri mazoezini na anaamini watakwenda kupeperusha vyema bendera ya nchi.

Pawasa alisema kabla ya kuondoka nchini wanatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki ili kujiimarisha zaidi na kurekebisha mapungufu ambayo yatakijenga kikosi chake.

**"Mechi hizo za kirafiki zitatusaidia kuona mapungufu na ubora wetu, tuongeze wapi baada ya kufanya mazoezi muda mrefu, sasa tunajipima kabla ya kuondoka kuelekea Afrika Kusini," alisema Pawasa.**

Kocha huyo, ambaye ni beki wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba alisema mechi hizo za kirafiki zitachezwa kati ya leo na keshokutwa na timu za hapa hapa nchini.

"Tumefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya mashindano haya, wachezaji wote wana molari makubwa na kuelekea kwenye michuano hiyo, tumejipanga imara kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania," Pawasa alisema.

Aliongeza wanataka kuendeleza heshima ya jina la Tanzania katika michuano hiyo inayoandaliwa huko Afrika Kusini.

"Matumaini yetu kuendelea kuipa heshima Tanzania, tayari COSAFA inajua ubora wa timu za Tanzania, hatutaki kushusha heshima, tutapambana kwa ajili ya taifa letu," alisema kocha huyo.

Kikosi hicho cha Tanzania kinakwenda kushiriki mashindano hayo kwa mara ya kwanza kikiwa ni timu mwalika kutoka kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.




Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (kushoto), akimvisha skafu ya Tanzania, mwigizaji mkongwe wa filamu za Kihindi, Sanjay Dutt, kutoka India wakati msanii huyo alipofanya mazungumzo na waigizaji wa hapa nchini na kuahidi kushirikiana nao katika kukuza tasnia hiyo kwenye hafla maalumu iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gwambina FC hali tete Championship

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 wiki hii na Kitayosce FC, timu ya Gwambina FC imeendeleza rekodi ya kutoshinda mechi hata moja tangu kuanza kwa Ligi ya Championship msimu huu ambapo imefikia raundi ya sita.

Gwambina iliyoteremka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliomalizika, iko katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi mbili.

Timu tatu za juu kwenye Ligi ya Championship yenye timu 16, zinatarajia kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu ujao, huku DTB ikiongoza baada ya kuichapa Ken Gold mabao 2-1.

Vinara hao DTB wameshinda michezo minne na kutoka sare mara mbili, hivyo wamejikusanya pointi 14 mpaka sasa.

Hata hivyo, timu nyingine ambazo zilishuka daraja kutoka Ligi Kuu, ambazo ni Ihefu na JKT Tanzania, zenyewe zinaonekana kupambana ili kujaribu bahati ya kurejea tena katika ligi hiyo ya juu nchini.



# *Dube akaribia kurejea dimbani*

**Na Saada Akida**

HALI ya mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube, haijaimarika na kwa sasa bado anaendelea kufanya mazoezi chini ya uangalizi wa madaktari wa timu hiyo kwa ajili ya kuhakikisha anapona kwa asilimia kubwa kabla ya kurejea kikosini.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati aliliambia gazeti hili mshambuliaji huyo anafanya mazoezi yanayoendana na matibabu ambayo yamewekwa katika programu maalum.

Vivier alisema wataendelea kumsubiria mshambuliaji huyo ingawa aliweka wazi anakaribia kurejea uwanjani.

"Msimu huu hatukuanza vizuri mechi za mwanzoni, haimaanisha kukosekana kwa Dube ni tatizo, kuna wachezaji mbadala wake na kumwacha nyota huyo apone kwa asilimia 100 awe fiti ndio jambo kubwa," alisema Vivier.

Aliongeza wametumia muda wa mapumziko ya kalenda ya kimataifa kufanyika kazi mapungufu yao na anaamini ligi itakaporejea watakuwa kwenye ushindani na wako tayari kukabiliana na hali hiyo.

Mechi inayofuata ya Azam FC itakuwa ni dhidi ya KMC FC na itachezwa Novemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.




Washindi wa Jackpot bonus kutoka kushoto ni Mohammed Mohammed, Deo Msemwa (katikati) na Yona Nyasomba wakishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni tano ambazo kila mmoja atapata baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA KUMPIKU RONALDO**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 28, anataka kuongeza mkataba wake na klabu hiyo, lakini mchezaji huyo wa Ufaransa anataka kumpiku, Cristiano Ronaldo na kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika Ligi Kuu England. ***(L'Equipe, via Metro)***

**STERLING AELEKEA BARCA**

BARCELONA inajiandaa kuimarisha safu yake ya ushambuliaji ifikapo Januari kwa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling, 26. ***(Mail)***

**CAVANI, WERNER SOKONI**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, 34, na nyota wa Ujerumani, Timo Werner mwenye miaka 25 wote wanawaniwa na Barcelona.

**MESSI KURUDI BARCA**

MSHINDI mara sita wa tuzo ya Ballon d'Or, Lionel Messi, 34, huenda akarudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona ifikapo Januari. ***(Daily Star)***

**VILLA KUILIPA RANGERS**

KLABU ya Aston Villa itawalipa Rangers takriban pauni milioni tatu kama watafikia makubaliano ya kumchukua, Steven Gerrard ili kuwa kocha wao mpya. ***(Times)***

**RABIOT ANUKIA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle ina hamu ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la Januari. ***(Calciomercato, via Mirror)***

**LIVERPOOL KUSAJILI WATATU**

LIVERPOOL inajiandaa kuwanunua wachezaji watatu katika dirisha la uhamisho la Januari ili kuziba pengo la Mohamed Salah, Sadio Mane na Naby Keita ambao watajiunga na timu zao za Taifa kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022). ***(Daily Star)***

**CARVALHO MAMBO BADO**

WAKALA Jorge Mendes anajaribu kumuunganisha kiungo wa kati wa Timu ya England, Fabio Carvalho, 19, na klabu ya Liverpool. ***(Daily Mail)***

**VLAHOVIC AKARIBIA JUVE**

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, 21, bado analengwa na Juventus, licha ya kuvutiwa na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu England. ***(Tuttosport)***

**BAYERN YAMFUATA CLEARY**

MASKAUTI wa Bayern Munich ya Ujerumani wanaendelea kumchunguza mshambuliaji wa West Brom mwenye umri wa miaka 17, Reyes Cleary ambaye amefunga mabao 12 msimu huu. ***(Daily Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA KUKOSA MECHI ZILIZOBAKIA ZA 2021

**Ni baada ya kiungo huyo kupata majeraha mazoezini akiwa na kikosi cha...**

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, anaweza kukosa michezo yote ya mwaka huu 2021 kutokana na majeraha aliyoyapata akiwa anajiaanda na majukumu ya kimataifa akiwa na Timu ya Taifa ya Ufaransa, imefahamika.

Taarifa zilizotoka kwenye kambi ya Timu ya Ufaransa kuhusu Pogba ni kwamba atakuwa nje ya uwanja akiuguza majeraha yake kati ya wiki sita hadi nane.

Ikiwa atakaa nje kwa wiki nane ina maana atakosa michezo miwili ya hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na pia atakosa karibu michezo 10 ya Ligi Kuu England iliyobakia kwa mwaka huu 2021.

**Pogba ambaye ilikuwa akose mchezo wa Novemba 20, mwaka huu ambapo Manchester United itakutana na Watford kutokana na kupewa kadi nyekundu kwenye mchezo uliopita walipovaana na Liverpool, sasa anaongeza orodha ya wachezaji majeruhi kwenye kikosi cha United.**

Ikumbukwe Manchester United kwa sasa ina wachezaji zaidi ya wanne ambao ni majeruhi na hawafikiriwi kurudi dimbani hivi karibuni.

Kikosi hicho cha Kocha, Ole Gunnar Solskjaer kinakabiliwa na wakati mgumu baada ya kufungwa na Liverpool mabao 5-0 na mwishoni mwa wiki iliyopita kilifungwa tena na wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City mabao 2-0.

Kwa sasa Manchester United ipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu England.

MECHI KALI
HOME
TANZANIA
2.85 | 2.99 | 2.41
DR CONGO
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 667

# ANCELOTTI HANA MPANGO KUINOA ITALIA



**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema hana mpango wa kuchukua mikoba ya kuinoa Timu ya Taifa ya Italia, kwani anafurahia zaidi kuendelea kuzinoa klabu.

Italia kwa sasa ipo chini ya mikono salama ya Roberto Mancini, ambaye aliiongoza kutwaa taji la Euro 2020.

Mkataba wa Mancini na Italia unamalizika mwaka 2026, huku akiweka rekodi ya kucheza mechi 37 bila kupoteza.

Ancelotti ambaye aliichezea Italia mechi 26 na kocha wa zamani wa Parma, Juventus, Milan na Napoli, aliulizwa kuhusu mpango wa kuinoa Italia ambapo alijibu hana mpango huo.

"Sijui, sijui kabisa," alisema Ancelotti akiiambia ESPN Colombia wakati Italia ikijiandaa na mchezo wa Kundi C wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Uswisi unaopigwa leo Ijumaa.

"Napenda kuendelea kuzinoa klabu na ndio kazi ninayopenda. Sijawahi kufikiria kuhusu timu ya taifa, na sina mpango huo."

Ancelotti amerudi kwa mara ya pili kuinoa Madrid baada ya kuiongoza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super, Klabu Bingwa ya Dunia na Copa del Rey wakati akiinoa kwa mara ya kwanza kati ya mwaka 2013 na 2015.



# Gerrard akaribia kutua Aston Villa

**LONDON,** England

STEVEN Gerrard ndiye kocha anayepigiwa chapuo la kuchukua mikoba iliyoachwa na Dean Smith katika klabu ya Aston Villa kwa sasa, na ni suala la muda tu kupewa nafasi hiyo rasmi.

Aston Villa imekuwa ikitafuta mrithi wa kuinoa klabu hiyo tangu imfukuze aliyekuwa kocha wake, Smith baada ya kupokea kichapo cha 1-0 kutoka kwa Southampton.

Gerrard amekuwa akipewa nafasi kubwa na kuwa chaguo la kwanza ambaye anaweza kuchukua mikoba hiyo, hasa kutokana na uhusiano mzuri na Mkurugenzi wa Aston Villa, Christian Purslow.

Wawili hao walikuwa pamoja kule Liverpool, ingawa Roberto Martinez, Paulo Fonseca, Kasper Hjulmand, Graham Potter na Ralf Rangnick nao wanapewa nafasi hiyo.

Mafanikio ya Gerrard akiwa na klabu ya Rangers yamewavutia mabosi wa Aston Villa baada ya kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Scotland pasipo kupoteza mchezo wowote msimu ulioisha mbele ya mahasimu wao Celtic ambao walichukua ubingwa mara tisa mfululizo.

**HABARI MICHEZO**


7,771,400

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/11/21 | 18:00 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.27 | 3.28 | 2.99 |
| 02. 13/11/21 | 18:00 | Tranmere vs Sutton United | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 03. 13/11/21 | 18:00 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 04. 13/11/21 | 18:00 | Bristol Rovers vs Northampton | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 05. 13/11/21 | 18:00 | Walsall vs Harrogate | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 06. 13/11/21 | 18:00 | Altrincham vs Boreham Wood | 2.83 | 3.27 | 2.35 |
| 07. 13/11/21 | 18:00 | Yeovil vs Eastleigh | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 08. 13/11/21 | 18:00 | Wealdstone vs Barnet | 2.43 | 3.41 | 2.63 |
| 09. 13/11/21 | 18:00 | Accrington vs Plymouth | 2.70 | 3.44 | 2.39 |
| 10. 13/11/21 | 20:15 | Mirandes vs Huesca | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 11. 14/11/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.13 | 3.18 | 2.24 |
| 12. 14/11/21 | 20:15 | Leganes vs Real Oviedo | 2.29 | 2.99 | 3.23 |
| 13. 14/11/21 | 20:15 | Burgos vs Ponferradina | 2.41 | 3.03 | 2.98 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 11 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1233 | Chiangmai United vs Khon Kaen United FC | 2.05 | 3.42 | 3.13 |
| 14:00 | 3471 | South Korea vs United Arab Emirates | 1.35 | 4.06 | 8.70 |
| 15:00 | 1341 | Port FC vs Ratchaburi | 1.67 | 3.61 | 4.43 |
| 15:00 | 3806 | Macedonia U21 vs Ukraine U21 | 3.38 | 3.24 | 2.02 |
| 15:00 | 4033 | Lebanon vs Iran | 9.44 | 4.05 | 1.34 |
| 15:00 | 4425 | Vietnam vs Japan | 14.40 | 6.15 | 1.15 |
| 16:00 | 1877 | Tanzania vs DR Congo | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 16:00 | 4513 | Uganda vs Kenya | 1.61 | 3.42 | 5.39 |
| 16:00 | 4988 | Ethiopia vs Ghana | 9.67 | 4.45 | 1.30 |
| 17:00 | 3031 | Baumit Jablonec vs Varnsdorf | 1.24 | 5.79 | 8.49 |
| 17:00 | 3851 | Maccabi Kishronot Hadera W vs MS Kiryat Gat W | 5.57 | 4.61 | 1.42 |
| 18:00 | 2373 | China vs Oman | 2.70 | 3.09 | 2.46 |
| 19:00 | 1411 | Malaga C.atco W vs Prainsa Zaragoza W | 2.05 | 3.48 | 3.09 |
| 19:00 | 2818 | Benin vs Madagascar | 1.55 | 3.56 | 5.77 |
| 19:00 | 5259 | Congo vs Namibia | 1.98 | 3.13 | 3.61 |
| 19:00 | 5745 | Rwanda vs Mali | 5.20 | 3.32 | 1.65 |
| 20:00 | 1377 | Iraq vs Syrian Arab Republic | 2.08 | 2.99 | 3.52 |
| 20:00 | 1758 | Croatia U21 vs Estonia U21 | 1.01 | 15.45 | 97.56 |
| 20:00 | 2242 | Armenia vs North Macedonia | 2.85 | 3.30 | 2.46 |
| 20:00 | 3625 | Georgia vs Sweden | 7.22 | 4.11 | 1.47 |
| 20:00 | 4163 | Azerbaijan vs Luxembourg | 2.50 | 3.05 | 3.00 |
| 20:00 | 4407 | Serbia vs Qatar | 1.49 | 4.20 | 6.60 |
| 20:00 | 5308 | Russia vs Cyprus | 1.15 | 7.23 | 18.07 |
| 20:30 | 1827 | Ukraine vs Bulgaria | 1.58 | 3.94 | 5.79 |
| 20:30 | 3369 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Bnot Netanya W | 1.17 | 7.14 | 9.65 |
| 20:30 | 3386 | Czech Republic vs Kuwait | 1.30 | 5.40 | 9.41 |
| 20:45 | 1267 | Hapoel Raanana W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.71 | 3.96 | 3.81 |
| 21:00 | 3739 | San Marino U21 vs Israel U21 | 87.03 | 15.47 | 1.01 |
| 21:30 | 2923 | San Martin Burzaco vs CA Atlas | 2.46 | 3.04 | 2.75 |
| 21:30 | 3541 | Hapoel Marmorek Rehovot vs AS Tel Aviv University W | 15.41 | 9.25 | 1.08 |
| 21:30 | 4119 | El Porvenir vs Lujan | 2.28 | 2.89 | 3.17 |
| 21:30 | 5459 | Leandro N Alem vs Claypole | 3.12 | 2.59 | 2.54 |
| 22:00 | 2549 | England U21 vs Czech Republic U21 | 1.50 | 3.96 | 5.60 |
| 22:00 | 3974 | Togo vs Senegal | 5.77 | 3.41 | 1.58 |
| 22:00 | 4527 | Hungary U19 vs Italy U19 | 5.41 | 4.35 | 1.46 |
| 22:00 | 4893 | South Africa vs Zimbabwe | 1.31 | 4.43 | 9.05 |
| 22:45 | 3180 | Malta vs Croatia | 22.96 | 8.19 | 1.12 |
| 22:45 | 3765 | Greece vs Spain | 7.42 | 4.21 | 1.45 |
| 22:45 | 3843 | Germany vs Liechtenstein | 1.03 | 13.29 | 59.80 |
| 22:45 | 4181 | France U21 vs Armenia U21 | 1.01 | 15.49 | 77.46 |
| 22:45 | 4426 | Slovakia vs Slovenia | 2.19 | 3.05 | 3.64 |
| 22:45 | 4508 | Ireland vs Portugal | 8.61 | 4.91 | 1.35 |
| 22:45 | 4828 | Romania vs Iceland | 1.60 | 3.90 | 5.60 |

### IJUMAA - 12 - NOVEMBA 2021

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 5963 | Ecuador vs Venezuela | 1.39 | 4.50 | 8.41 |
| 01:00 | 2359 | Ponte Preta vs Botafogo RJ | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 01:00 | 2386 | Flamengo vs Bahia BA | 1.39 | 4.43 | 6.55 |
| 01:00 | 3237 | Sampaio MA vs Vila Nova GO | 2.95 | 2.90 | 2.41 |
| 02:00 | 1738 | Paraguay vs Chile | 2.58 | 3.03 | 2.93 |
| 03:00 | 1370 | Estudiantes Rio Cuarto vs Temperley | 2.31 | 2.79 | 3.23 |
| 03:30 | 1763 | Brazil vs Colombia | 1.46 | 4.29 | 7.18 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RAMOS RASMI KUANZA MAZOEZI



**PARIS,** Ufaransa

SERGIO Ramos anajindaa kurudi mazoezini baada ya kuwa nje kwa muda mrefu kutokana na majeruhi, tangu asajiliwe na Paris Saint Germain na hajacheza mchezo wowote hadi sasa.

Sergio aliachana na Real Madrid na kuhamia kwa matajiri wa jijini Paris kwa uhamisho huru kwenye majira ya joto baada ya kumaliza mkataba wake na klabu hiyo aliyokaa nayo kwa takribani miaka 16.

Ramos alijiunga na PSG akiwa bado anauguza majeraha yake ambayo yalimweka nje na kumfanya akose michezo takribani 30 ya msimu uliopita na hadi sasa hajacheza mchezo wowote.

Sergio sasa amekosa michezo 13 ya Ligue 1, kwa taarifa zilizopo kwenye kambi ya PSG ni kuwa ameanza kufanya mazoezi na wachezaji waliobaki na anatarajiwa kuungana na nyota wengine baada ya kumalizika kwa kalenda ya kimataifa.



# Chiellini aondolewa kikosi cha Italia

**ROME, Italia**

MLINZI mkongwe, Giorgio Chiellini ameondolewa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Italia kinachojiandaa na mchezo wa Kombe la Dunia nchini Qatar baada ya kushindwa kupona kwa wakati majeraha yake.

Chiellini alikuwa ni mmoja wa wachezaji muhimu ambao watakosa michezo ya kufuzu Kombe la Dunia la mwaka 2022.

Shirikisho la Soka la Italia limesema nahodha na mlinzi huyo wa kati hatakuwapo kwenye mechi mbili za Italia za kufuzu kwa michuano ya Kombe la Dunia.

Chiellini ataukosa mchezo wa leo Ijumaa utakaopigwa jijini Roma dhidi ya Uswisi kwenye Kundi C, ambapo Italia wana alama sawa na wapinzani hao lakini wanaongoza kundi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Roberto Mancini amepoteza wachezaji wawili ndani ya saa 24 ambao ni Chiellini na Ciro Immobile na bado ana wasiwasi wa kumpoteza tena kiungo wa Inter Milan, Nicolo Barella.

# Michezo

Ijumaa Novemba 12, 2021

Nipashe



Gerrard akaribia kutua Aston Villa UKURASA 21



Beki wa Taifa Stars, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' (kulia), akijiandaa kumtoka mshambuliaji wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Arsene Zola katika mechi ya Kundi J iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Stars ililala mabao 3-0. **PICHA: TFF**

## Pablo kuliamsha Simba

**Na Saada Akida**

KAZI imeanza! KOCHA Mkuu mpya wa Simba , Pablo Franco anatarajia kuanza rasmi kazi leo kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting na mchezo wa kimataifa wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa baadaye mwezi huu na Red Arrows kutoka Zambia.

Ruvu Shooting itawakaribisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Simba ifikapo Novemba 19, mwaka huu kwenye dimba la CCM Kirumba, jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana alisema Pablo amefurahishwa na mapokezi aliyopata kutoka kwa wenyeji wake na ameweka wazi anatarajia kupata ushirikiano ili kupata mafanikio.

Hitimana alisema baada ya kufika kwenye mazoezi ya timu hiyo jana asubuhi, na kuangalia programu zilizokuwa zinaendeshwa na wasaidizi wake, yeye aliweka wazi ataanza kibarua chake leo.

Kocha huyo alisema Mhispania huyo amewaeleza anaamini Simba itafikia malengo yake kwa kuhakikisha kikosi kinakuwa imara na bora wakati wote wa msimu.

"Kocha Mkuu amekuja, tumetambulishwa na alifika katika mazoezi ya leo (jana) asubuhi, hakutaka kuingilia kile tulichokuwa tunafanya na kutueleza tunatakiwa kuendelea na programu tulizokuwa tukifanya na yeye ataanza rasmi kesho (leo) asubuhi," alisema Hitimana.

Aliongeza ana imani ujio wa kocha huyo utashusha 'presha' ya mafanikio iliyopo katika kikosi pamoja na wanachama na mashabiki wa Simba.

# Taifa Stars yajiweka mtegoni

## Samatta aangua kilio baada ya bao la tatu...

**Adam Fungamwangwo na Saada Akida**

NAHODHA wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, aliangua kilio baada ya timu yake kufungwa bao la tatu na wapinzani wao kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), katika mechi ya Kundi J iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana.

**Hadi dakika 90 zinamalizika, Stars ilikubali kichapo cha mabao 3-0 na kuifanya DRC kupanda kileleni kwenye kundi hilo kwa kufikisha pointi nane, kabla ya mechi ya usiku ambapo Benin waliikaribisha Madagascar.**

Mabao ya Gael Kikuta, Nathan Indumba na Ben Malango Ngita, yaliiweka 'miba' njiani kwenye safari ya Taifa Stars kuelekea katika fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Qatar mwakani.

Kinakuwa ni kipigo cha pili nyumbani kwa Stars katika mashindano hayo baada ya kufungwa bao 1-0 na Benin katika mechi iliyochezwa Oktoba 7, mwaka huu, ikiwa ni matokeo yaliyowachanganya Watanzania ambao waliohudhuria uwanjani au waliokuwa wakitazama kwenye televisheni.

Stars ilianza pambano hilo kwa kasi na kama ingekuwa makini ingeweza kupata mabao mawili ya haraka dakika ya pili na dakika ya nne kupitia kwa Simon Msuva, baada ya kugongeana na wenzake, kabla ya kuingia kwenye eneo la hatari na kupiga shuti lililotoka nje kidogo ya lango la DRC.

Dakika mbili baadaye, Msuva akiwa umbali ya takribani mita 35 alipiga shuti kali, lakini nalo likatoka nje kidogo la lango na baada ya kosa kosa hizo mbili, wageni waliamka na kuanza kuonyesha 'ukubwa' kwa kufanya mashambulizi ya hatari ambayo baadaye yalizaa matunda.

Alikuwa ni Kakuta, aliyepewa pande maridadi na Mbokani, kabla ya kuachia kombora lililomshinda kipa wa Stars, Aishi Manula kudaka na kujaa wavuni.

Bao hilo lilionekana kuwachanganya wachezaji wa Stars na kuanza kucheza kwa papara, bila ya kuwa na utulivu, hali iliyosababisha wakose mabao mengi ya wazi.

Faulo iliyopigwa na Mbwana Samatta dakika ya 13, iliyotoka na Feisal Salum kufanyiwa madhambi, nusura iliipatie Stars bao, lakini mpira ukatoka sentimeta chache huku krosi ya Kibu Denis iliwapita Msuva na Samatta dakika ya 16 na kuikosesha Tanzania nafasi ya kusawazisha.

Shuti la Fei Toto lililokuwa limewapita wachezaji wote wa DRC na kipa wao, Joel Kiassumbua lililoonekana linajaa wavuni, lilimbabua Samatta na kurejea uwanjani dakika mbili baadaye.

Kibu aliukosa mpira wa krosi iliyopigwa na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' dakika ya 23, na kuendeleza mlolongo wa kukosa mabao ya wazi.

Kipindi cha pili, ilifanya mabadiliko mengi ya kuwatoa Dismas Novatus, Kennedy Juma, Kibu Denis, Feisal Salum na Shomari Kapombe na kuwaingiza Reliants Lusajo, Mzamiru Yassin, Salum Aboubakar, John Boccon, Kibwana Shomari na Erasto Nyoni, lakini hayakusaidia kitu.

Wakati Stars ikitafuta bao la kusawazisha, ilijikuta ikishindiliwa bao la pili dakika ya 65 lililofungwa na Indumba, ambaye alifunga kirahisi akiwa hajakabwa, baada ya DRC kupasiana kona fupi, kabla ya mpira kumiminwa golini.

Dakika tano kabla ya mechi kumalizika, Ngita alifunga bao la tatu kwa kichwa akiunganisha krosi ya Ngonda Muzinga.

Nafasi kubwa pekee kwa Stars kufunga bao ilikuwa ni dakika ya 77, Nyoni alipopiga kichwa mpira ukagonga mwamba wa juu, kabla ya kutokea kizazaa na kipa, Kiassumbua akawa shujaa kwa kuupangua mpira uliotoka nje na kuwa kona tasa.

Stars inayonolewa na Kim Poulsen inatarajiwa kusafiri kuwafuata wenyeji wao Madagascar katika mchezo wa mwisho wa Kundi J utakaochezwa keshokutwa nchini humo.

### PABLO ATINGA UWANJANI

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, aliungana na mashabiki wa soka nchini kuishaingilia Stars ukiwa ni mchezo wake wa kwanza anauona mubashara kwenye ardhi ya Tanzania.

Wakati wa mapumziko, Pablo alinyanyuka katika kiti alichokaa na kuwasalimia kwa kuwapigia makofi mashabiki waliokaa eneo ambalo hupendwa kutumiwa na wanachama na mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi.

Kitendo hicho kiliamsha furaha na mashabiki hao wachache waliofika uwanjani kuishangilia Stars.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >